# *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa*

Habari za jioni, marafiki. Ni majaliwa makubwa kurudi hapa kwenye jumba la mikutano tena, usiku wa leo, ama, nyumba ya uwanjani. Nasi tuna furaha sana kuwa na fursa hii ya kuzungumza nanyi tena, lakini natumaini si muda mrefu kama nilivyofanya jana usiku.

Mwanangu alikuwa akizungumza na baadhi ya wahudumu, nao wakasema, "Ndugu Branham huzungumza kwa kama muda gani?"

Akasema, "Loo, si muda mrefu sana, mpaka atakapozungumzia somo la Ibrahimu, wakati mwingine anaweza tu ku—kupotea tu."

2 Na jana usiku nilikuwa hapa yapata saa mbili na dakika arobaini na tano. Mtu fulani alimwambia asubuhi ya leo, kasema, "Ibrahimu atakuwa nini? Lazima iwe ni kitu fulani!"

3 Ninyi ni watu wazuri sana, nami ninapenda kuzungumza na watu ambao Neno linaitikia, kuona watu wa thamani wakimjia Bwana, inaifanya nzuri sana, ni moja ya furaha kuu sana moyoni mwangu.

4 Ninakumbuka wakati mmoja nilipokuwa mhudumu kijana. Mimi . . . Kulikuwa na rafiki yangu mwingine mhudumu, dada yake, nilimpeleka nyumbani baada ya kanisa usiku mmoja. Tulikuwa tukipanda barabarani, naye kwa namna fulani alikuwa Mkristo wa kawaida, wa jina tu, vile ningesema, nami niliamini ya kwamba alimwamini Kristo, na kadhalika, lakini hakuwa ameingia kindani kama vile ninavyofikiri Mkristo anapaswa kwenda kukiri Ukristo, ba—basi akasema, "Vipi kesho usiku, kwenda kwenye sinema?"

Nikasema, "Siendi kwenye sinema."

Naye akasema, "Vema," kasema, "wana uwanja wa kuteleza kwenye barafu hapa chini, vipi kuhusu kwenda kuteleza kwenye barafu?"

Nikasema, "Siendi kuteleza kwenye barafu."

Akaniomba niende sehemu tatu ama nne mbalimbali, nami nikasema, "Sifanyi hivyo."

Akasema, "Vema, kama kijana mwanamume hapa, yapata umri wa miaka ishirini na miwili, unapata wapi raha yako?"

Nikasema, "Katika nyumba ya Bwana." Nikasema, "Hiyo . . . "

5 Basi siku chache usiku baada ya hapo nilikuwa kanisani, naye huyo msichana alikuwa ameketi hapo nyuma, na—na kwa hiyo usiku huo nikafanya wito wa madhabahuni, na yapata watu ishirini wakaja madhabahuni, wakilia, vijana. Nami nikamwashiria, nikasema, "Ninapata raha zaidi kutoka kwa hilo, kuliko yote ambayo ulimwengu ungeweza kutoa." Ni kitu ambacho unajua u—unahisi unapolala chini usiku umefanya jambo fulani, kujaribu kumsaidia mtu fulani. Hilo ndilo lililotuleta hapa, kujaribu kufanya mizigo ya maisha iwe myepesi kidogo kwenu, mnaona, na—na kuwasaidia wale wasiomjua Kristo kumjua.

6 Nikiwaombea wagonjwa, nilikuwa nikipanda vipandio, nami nikawasikia wakitaja kuhusu Ijumaa usiku kwa ajili ya magonjwa ya dharura. Vema, hiyo ni kweli, tunaposhuka na kuombea visa vyote vya dharura, wametenga usiku huo, bila shaka, kwa ajili ya jambo hilo.

7 Sasa, uponyaji wa Kiungu hautegemei, kumbukeni, kuwekewa mikono, hilo ni sawa. Sasa, hao ni Wamarekani, inawabidi kuwekewa mikono, la sivyo kamwe hawaamini, hivyo tu, huna budi kuwagusa kwa njia fulani, na, la sivyo hai—haifai kitu.

8 Na, lakini sasa, kama mtanivumilia tu kwa dakika moja, si kuwa tofauti, lakini hivyo sivyo Mungu anavyowashughulikia Mataifa, hayo yalikuwa ni mapokeo ya Kiyahudi. Mnakumbuka, yule Myahudi alimwambia Yesu, "Binti yangu anasumbu-. . ., uh, mgonjwa sana, naye yuafa." Kasema, "Njoo, uweke mkono Wako juu yake, naye atapona." Kiyahudi.

Lakini wakati . . . alipoenda kwenye nyumba ya Mrumi, yule Mmataifa, alisema, "Hata sistahili Wewe kuja chini ya paa langu, nena tu Neno." Mnaona?

Ndipo Yesu akawageukia Wayahudi, na kusema, "Sijaona imani kama hiyo katika Israeli." Mnaona?

9 Sasa, huyo Mrumi alisema nini? "Mimi ni mtu niliye chini ya mamlaka, na mimi ni akida." Hiyo ilimaanisha alikuwa na watu mia moja, *karne nzima*, watu mia moja chini yake. Basi akasema, "Na—na—namwambia mtu *huyu*, 'Nenda,' naye anaenda; mtu *huyu*, 'Njoo,' naye anakuja." Kwa nini? Alikuwa juu yao, alikuwa bwana juu yao. Naye alisema nini kwa kumwambia Yesu hivyo? Kwamba Yeye alikuwa Mtawala, angeweza kuyatawala magonjwa yote, na chochote alichosema ilibidi kiwe. Loo, hiyo si ni njia halisi ya kukabiliana nalo? "Wewe sema tu mwanangu yu hai, naye ataishi. Nena tu Neno, hilo tu ndilo unalopaswa kufanya."

10 Sasa, Durban, Afrika Kusini, hivi majuzi, sijui kama hao wavulana wamewahi kukitoa kitabu hicho bado ama la, juu ya Afrika, kilichoandikwa na Kapteni Julius Stadsklev, tulikuwa tumeingia, huko Durban, Afrika Kusini, ambako tulikuwa na

mikutano huko Johannesburg, na, loo, jamani, mambo kama hayo ambayo yangechukua saa kadhaa kusimulia aliyofanya Bwana.

11 Lakini tulipoenda Durban, kamwe sisahau, Sidney Smith, meya wa Durban, alikuja na kunichukua, naye akasema, “Loo, Ndugu Branham,” kasema, “hii ni historia ya Afrika.” Akasema, “Wewe . . . ” Kasema, “Wamekuwa wakimiminika huku kwa yapata siku tano, na,” kasema, “zimesalia siku nne ama tano, bado.” Wakiwaleta wapendwa wao kwa mkokoteni wa kujitengenezea, jinsi wangeweza kubebana. Ndipo simba anapokuja, wanawasukumia juu ya mti mpaka simba aondoke, kisha wanashuka, wanawaleta, wakijaribu kuwapeleka mikutanoni. Kwa kuwa walikuwa wamesikia yale Bwana aliyofanya mahali pengine, Johannesburg, na—na halafu uwe Chelan, na sehemu nyingi.

12 Na kwa hiyo, nami nawaambia, Ukristo katika Afrika ni kitu kinachodhoofika, bila shaka ni dhaifu, kwa sababu tumefundisha kusoma, kuandika, na hesabu, badala ya kufanya yale Yesu aliyotuambia tufanye, Yeye alisema, “Enendeni ulimwenguni kote, mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Sasa, Yeye kamwe hakusema, “Enendeni mkafundishe Neno.” Alisema, “Hubirini Injili.” Nayo Injili ni dhihirisho la Kristo aliyefufuka, huyo ni Roho Mtakatifu. Paulo alisema, “Injili inakuja si kwa Neno tu, bali kwa nguvu, madhihirisho, uthibitisho wa Roho Mtakatifu.” Ingebidi iwe kusudi itimize Marko 16.

13 Nami nilikuwa nikitoka nje, mimi na Bw. Sidney Smith, meya wa Durban, tukienda kwenye uwanja wa mashindano ya farasi ambako . . . Ndio uwanja wa pili ulio mkubwa sana ulimwenguni. Na basi hao hapo . . . Mahali pote palikuwa pamejaa watu, kote kote humo uwanjani, kisha mahali pengine pakajengwa upande wa pili. Hiyo ilikuwa tu ni siku yetu ya pili kule, tulikuwa tumebakisha siku moja. Ilikuwa Jumapili alasiri.

14 Loo, mnajua jinsi watu wanavyoweza kutoa hesabu ya kiinjilisti ya kufikia, baadhi yao, “nusu milioni,” mnajua jinsi wanavyofanya. Na, kwa hiyo ni . . . Nilikadiria kidogo sana kuliko vile walivyosema watu walikuwa.

15 Lakini siku hizi watu wanajaribu kuona ni watu wangapi unaoweza kuwaleta huko nje, hilo halina uhusiano wowote nalo. Ni kama Kristo yupo mle ama hayupo, mnaona, hilo ndilo jambo muhimu. Na, ni, afadhali niwe peke yangu na niwe pamoja Naye, kuliko kuwa pamoja na milioni kumi Naye hayupo. Mimi . . . Ni popote tu Yeye alipo, na hilo ndilo jambo muhimu, si ati ni nani anayeweza kupata umati mkubwa zaidi, na kuuanika magazetini na yote hayo. Mbona, kanisa Katoliki linaweza kutushinda sisi sote kwa jambo hilo. Marekani, Bw.

Rais Kennedy angeweza kuwashinda hao wote, nadhani, huku Marekani.

16 Kwa hiyo si umati, Mungu haishi katika umati, Yeye huishi katika mioyo minyenyekevu, hapo ndipo Yeye alipo. "Walipo wawili watatu wamekusanyika katika Jina Langu, nitakuwa katikati yao." Hilo ndilo tunalotaka kuangalia, si mambo makuu, ya kuvutia sana, bali u—uhalisi wa Bwana Yesu aliyefufuka.

17 Sasa, halafu katika mkutano huu niliona wengi sana wao kule waliokuwa na vinyago vidogo kooni mwao. Hawakuvaa nguo zozote, wengi wao, walikuwa wenyeji wasiostaarabika. Na kwa hiyo, nikasema, "Hivyo vibandiko kwenye koo lao ni vya nini?"

Akasema, "Loo, huko ni kutiwa alama, wao ni Wakristo."

Nikasema, "Na kubeba sanamu?"

"Loo, naam, wanabeba sanamu, kwa vyovyote vile."

18 Na sasa, hizo ndizo nguvu za *unaoitwa* Ukristo. Na kwa hiyo mimi. . . Wanafanya nini? Mama fulani anamtuma mtoto wake huko awe mmishenari, na kufikiri angekuwa David Livingstone, basi inakuwaje? Yeye anaishi katika hoteli ya fahari sana, na gari zuri la kuendesha kwenye boma, wanacheza maskini dansi ndogo huko nje wakati wanapowaleta kutoka kwenye migodi ya almasi, na kuwasambazia vitini kadhaa. Wanajua nini kuhusu hicho?

19 Lakini siku za David Livingstone sio sasa, hao hawarudi misituni. Na hizo ndizo nguvu za wamishenari katika nchi za kigeni, wakijaribu kuwaelimisha, ma-ABC. Nawe unafanya nini? Unawafanya mtoto maradufu, zaidi, wa kuzimu kuliko walivyokuwa walipoanza. Wanafika katikati ya mji, inawabidi wanawake kubeba bunduki kwenye pochi zao, wasije wakabakwa. Wakati akiwa huko nje katika kabila, katika hali yake ya kikabila, yuko sawa, kitu pekee anachohitaji ni Kristo, kwa sababu yeye ana—yeye ana sheria za kikabila ambazo zitaushinda Ukristo vyovyote utakavyouchukua.

20 Kwa mfano, katika kabila moja kule, kama msichana hajaolewa mpaka amefikia umri fulani, ha—hana budi—hana budi kufutilia mbali rangi ya kikabila, kwa sababu amefedheheshwa. Na kabla hajaolewa, anachunguzwa ubikira wake, kama akipatikana na hatia, hana budi kumsema mwanamume aliyetenda hilo, wote wawili wanauawa pamoja. Vipi kama hilo lingefanyika Marekani? Kungetokea maafa mengi, sivyo, miongoni mwa *wanaojiita* Wakristo? Mnaona, kwa hiyo hawahitaji uadilifu, wanachohitaji ni kumjua Mwokozi.

21 Kwa hiyo hao hapo, wakimiminika mle. Na kuna jamaa mmoja kule, na, jamaa mdogo, akienda pale akiwa na sanamu mkononi mwake. Nami nikasema. . . Akasema, "Je, ungependa

kuzungumza naye?" Kasema, "Yeye ni—yeye ni Mshangaani." Wana Xhosa, na Washangaani, na Wabasuto, na Wazulu, na makabila mengi sana mbalimbali. Naye akasema—akasema, "Yeye ni Mshangaani, ninaweza kuzungumza lugha yake." Kasema, "Mwite chochote utakacho, nitakutafsiria."

22 Basi meya akaendesha gari lake pale. Nikasema, "Halo, Thomas," nilimwita Thomas kwa sababu ni Mkristo aliyebeba sanamu. Nami nikasema, "Halo, Thomas." Nikasema, "Je, wewe ni Mkristo?"

"Naam." Alimwamini Amoyah. *Amoyah* ni neno, linatokana na "nguvu zisizoonekana" kama upepo, Amoyah. Alimwamini Amoyah.

Nikasema, "Kwa nini unaibeba hiyo sanamu basi?"

23 Vema, alikuwa na sababu nzuri, baba yake aliibeba. Siku moja simba alimwandama baba yake, akaiweka maskini hiyo sanamu chini, akawasha moto, kisha akakariri maombi aliyoambiwa na mchawi, huyo simba akaogopa, na kukimbia.

24 Nikasema, "Mimi ni leeujagter." *Leeu* ni "simba," *jagter* ni "mwindaji." Nikasema, "Mimi huwawinda simba, na ninajua tabia zao. Hayo maombi, wala ile sanamu haikumfukuza huyo simba, moto ndio ulimwogopesha, mnyama huogopa moto." Loo, vema, angeibeba kwa vyovyote vile, endapo—endapo Yule Asiyeonekana atashindwa, huyu asingeshindwa, kwa hiyo hizo hapo nguvu za Ukristo.

25 Lakini wakati siku hiyo, wakati huo mkutano ulipoanza, nilimtuma Billy aende akasambaze kadi za maombi. Loo, rehema! Kamwe usingeweza kuwazia juu ya kitu kama hicho. Hata karibu hakuwa na angalau nguo yoyote alipotoka nje.

26 Hao watu, nao iliwabidi kuwa nao, nina picha yake ya rangi, ambapo walikuwa wamewazungushia nyua kwa makabila, maelfu mara maelfu. Nilikuwa na wakalimani kumi na watano, wakati ningesema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu," ningeenda kunywa maji, kisha niketi chini, mpaka mmoja . . . Nilikuwa nikiwasikia Wapentekoste wakinena kwa lugha, nami nikawazia, "Jamani, hiyo haiwezi kuwa sahihi." Lakini baada ya siku hiyo nikatambua ilikuwa sahihi. Hakuna sauti inayoweza kutolewa, isiyokuwa na maana, mwajua, ninaamini Biblia ilisema kitu kama hicho, "Hakuna sauti isiyo na maana." Mnaona, ninii, kwamba kuna maana ya kila sauti ya kitu fulani. Baragumu ikitoa sauti isiyojulikana, mnaona hilo.

27 Kwa hiyo mmoja wao angesema, ningesema, "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu," mmoja wao angesema " . . . ? . . . " [Ndugu Branham anamwiga mkalimani Mwafrika—Mh.] Mwingine aseme, " . . . ? . . . " Hiyo ni, "Mwana wa Mungu, Yesu Kristo." Na—na hao wengine wangetoa kila namna ya minong'ono ya kigeni kooni mwao, kama ndege, lakini hiyo ilimaanisha "Yesu Kristo, Mwana wa Mungu." Ilitafsiriwa kwa makabila yao ya

Waislamu elfu kumi kule. Na kwa hiyo, halafu hao ni wale wanachukuliwa kuwa ni wagumu, wametokana na Wamedi na Waajemi wa kale, ambao hawabadiliki, wala hawageuki.

28 Na kwa hiyo nilikutana na mmishenari mmoja, akasema, "Wazia hilo, Ndugu Branham, Nimekuwa hapa miaka thelathini nami nikapata kito kimoja cha thamani."

Nikasema, "Ni kitu gani hicho?"

"Nilimleta Mwislamu mmoja katika Ukristo." Sasa, hilo kweli ni jambo kubwa kwa—kwa mmishenari kumgeuza Mwislamu akaingie katika Ukristo.

29 Kwa hiyo siku hiyo wakati...Nikasema, "Vema sasa, hatuwezi kuwa na kadi za maombi kuwapanga watu mstarini, kwa hiyo nitamwomba mmishenari wa kila kabila achukue angalau mmoja au wawili kutoka katika kila kabila, na kuwaleta hapa jukwaani." Vema, walikuwa wamejenga jukwaa, kitu kirefu kuliko *hili*, refu kidogo, kote kote kwenye huo uwanja wa mashindano ya farasi, spika kubwa zimewekwa kutoka kila mahali.

30 Nami nikasema, niliwanukulia hadithi ya Yesu, Nikasema, "Sasa, kuhusu uponyaji, ama wokovu, hilo ni jambo ambalo tayari amekufanyia, ni wako, inakubidi tu kuukubali, uponyaji wa Kiungu vivyo hivyo. Lakini swali lililo moyoni mwako," nikasema, "labda, kama tu ilivyo katika, karibu mioyo yote ya Wamarekani, na kadhalika, kila mahali: Je, Yeye kweli yu hai, ama hivi—hivi yale mapokeo ya Kiyahudi kwamba 'Walimwiba kaburini, na kumchukua,' ndi—ndivyo hivyo?" Kasema, "Hilo ndilo mnaloshangaa."

31 Nikasema, "Sasa, jambo ni kwamba Yeye anadai kuwa, Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Basi iwapo ndivyo alivyo, si atafanya kama alivyofanya jana?" Na kuwapa tu hadithi dhahiri. Ilinichukua kama saa moja kufanya hivyo, kuzungumza tu, kuwaletea jambo hilo. Hatimaye, walikubali.

32 Vema, hao wamishenari waliwapanga watu mstarini. Kulikuwa na yapata madaktari wanane ama kumi wa tiba, na kulikuwa na madhehebu ya kila namna yaliyolundikana kule kutoka kila mahali.

33 Na huko kwenye uwanja wa vita, hatuulizi, "Je, wewe ni Mmethodisti? Wewe ni Mbaptisti?" Ndugu, ni kujaribu kuwaleta makafiri kule, hivyo tu. Hata makasisi wa Katoliki walikuwa pale wamevalia, si kama kasisi wa Katoliki, bali wamevaa nguo kama za hao wenyeji. Mnaona, uko kwenye uwanja wa vita basi.

34 Kama tu nilivyosema jana usiku, tukienda vitani, husemi, "Je, wewe ni Mhoosia? Je, wewe ni msaga mahindi? Wewe ni nani?" Hilo halileti tofauti yoyote, tuko kwa ajili ya jambo moja, hilo ni kwa ajili ya taifa. Hivyo ndivyo tunavyosimama katika Ukristo. Hivyo ndivyo tunavyopaswa kusimama nyumbani,

namna hiyo, tungekuwa na nafasi kubwa zaidi ya kupigania, kama tu tungefanya hivyo.

35 Na kwa hiyo, basi wakati ninii . . . Wa kwanza kuja alikuwa ni mwanamke wa Kiislamu, nami nikasema, “Unazungumza Kiingereza?”

“La.”

36 Kwa hiyo mkalimani wa Kiislamu akaja. Na kwa hiyo, mwanamke huyo alikuwa ni wa ukoo safi, ametiwa nukta katikati ya macho, na kadhalika, kwa nukta nyekundu, ambayo inamaanisha yeye ni Mwislamu kwelikweli, na anamkana Kristo. Kwa hiyo, nikasema, “Vema, kwa nini unanijia, nikiwa Mkristo? Wewe, ukiwa ni Mwislamu, kwa nini hukumwendea shekhe wako?”

37 Loo, wao ni, wanamwamini Mungu, hao ni watoto wa Ishmaeli. Kila asubuhi king’ora hicho kikubwa kinasikika huko nje, ndipo shekhe anajitokeza na kusema, “Kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai.” Hiyo ni kweli. “Naye Muhammad ndiye nabii Wake.”

Tunaamini kuna Mungu mmoja wa kweli na aliye hai, naye Yesu ndiye Mwanawe.

38 Nao wakasema, “Na iwe mbali na Mungu kuwa na Mwana, Roho kuwa na mwana.” Kwa hiyo hawaamini hilo. Kwa hiyo basi, bila shaka, hawana budi kuwa hivyo, wao ni watoto wa Ishmaeli.

39 Kwa hiyo basi—kwa hiyo basi wakati huyu, mwanamke huyu, nilisema, “Kwa nini hukwenda kwa shekhe wako?”

Akasema, kupitia kwa mkalimani, kila mara, alisema, “Na—naamini ya kwamba ungeweza kunisaidia.”

Nikasema, “Umewahi kusoma Agano Jipya?”

Akasema, “Nimelisoma.”

40 Nami nikasema, “Basi kama umesoma Agano Jipya, kama Yesu Kristo ndiye yule Nabii aliyenenwa kwamba angekuja, na Musa, alinena juu ya Nabii atakayekuja, je, Yeye angekuwa ni nabii?”

Akasema, “Kweli angekuwa.”

41 Nikasema, “Basi kama Yeye alikufa na kufufuka tena . . . Mungu wenu, nabii wenu amekufa na kuzikwa, na yuko kaburini mwake kwa muda wa miaka elfu mbili.” Wanabadilisha walinzi kila baada ya saa nne, nimekuwa huko, farasi mweupe, wakimtarajia kuja, na kuuteka ulimwengu. Lakini nikasema, “Amekufa, kaburi Lake liko huko naye amezikwa humo ndani, naye ameenda.” Kisha nikasema, “Lakini Bwana wetu, Masihi, Nabii wa Mungu,” nikasema, “Mwana wa Mungu, wakati alipokuwa humu duniani, Yeye, alipoondoka, alimtuma Roho Wake Mtakatifu juu ya Kanisa kufanya mambo yale yale

aliyofanya Yeye, na kuonyesha ya kwamba Yeye angali alikuwa ni Nabii miongoni mwao." Nikasema, "Unaamini hilo?"

Akasema, "Kama ndivyo ilivyo, ninaamini."

42 Nikasema, "Basi kama Mwislamu kwa Mkristo, ama, Mkristo kwa Mwislamu," nikasema, "ninyi, labda, nasema katika sehemu hii wote ni Waislamu, kuna angalau elfu kumi wenu mlioketi hapa ndani." Nikasema, "Mwanamke huyu, siwezi kuzungumza lugha yake. Lakini, sasa, kama Yesu huyu ni Masihi, na Masihi, kama nilivyowanukulia kutoka katika Biblia yale aliyofanya alipokuwa hapa duniani kuthibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, nao wakashindwa kutambua hilo, ni wale tu waliokusudiwa Uzima," Nikasema, "basi kama Yeye angekuwa hai, na angeahidi ya kwamba kazi alizofanya sisi nasi tungezifanya, mngeamini hilo, ninyi Waislamu?" Nao wakainua mikono yao.

43 Kwa hiyo nikamgeukia na kusema, nikaangalia na kuona ono, nikasema, "Sasa, mume wako ni mtu mfupi, ana masharubu meusi. Na jina lako ni . . . " Ilinibidi kuliendelezea herufi, nisingeweza kulitamka.

Ndipo akainua mkono wake, "Hiyo ni kweli."

44 Nikasema, "Ulikuwa katika ofisi ya daktari hivi majuzi, huyo daktari alikuwa na upara, naye hakuwa mzee sana, alikuchunguza, naye akasema ulikuwa na uvimbe, ama, uvimbe maji kwenye titi lako la kushoto. Mumeo alikungojea kwenye ukumbi."

Ndipo machozi yakitiririka mashavuni mwake, akasema, "Hiyo ni kweli."

Nami nikasema, "Sasa, nini . . .? Je, unamkubali Yesu kama Mwokozi wako?"

Akasema, "Sasa ninamkataa Muhammad, na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu."

Nikasema, "Basi, katika Jina la Yesu Kristo, ninakutangaza kwamba umeponywa. Nenda, hebu daktari wako akuchunguze, na aniletee ushuhuda wake."

45 Aliyefuata alikuwa ni mwanamke ambaye alikuwa ni mwanamke mzungu, alikuwa Mwafrikana. Sasa, kuna tofauti kati ya *Afrika*, huyo ni mtu mweusi, *Mwafrikana* ni Kaburu, mzungu huko Afrika. Nami nikasema, "Je, unazungumza Kiingereza?" Ni nchi yenye lugha mbili.

Naye akasema, "Ninakizungumza."

Ndipo nikasema, "Basi unaamini ya kwamba Mungu alimtuma Mwanawe kufa badala yako?"

Akasema, "Mimi ni Mkristo, Bw. Branham."

Nami nikasema, “Vema, basi unaamini mimi ni mtumishi Wake?” Inakubidi kuangalia maneno unayowaambia. Nami nikasema, “Unaamini hilo?”

Akasema, “Ninaamini hadithi niliyosoma katika kitabu chako ni ya kweli. Ninaamini ya kwamba wewe ni mtumishi wa Mungu.”

46 Nikasema, “Basi, kama mimi ni mtumishi wa Mungu, kama ningeweza kukuponya, wala nisingekuponya, ningekuwa m—mtu mbaya sana, kama ningeweza kukusaidia kwa njia yoyote.” Kisha nikasema, “Njia pekee ninayoweza kukusaidia ni kupitia karama ya Kiungu. Kama Yeye angalikuwa amesimama hapa, Mwenyewe, asingeweza kufanya cha zaidi, kwa sababu kuhusu uponyaji wako, na kadhalika, Yeye tayari ameufanya.” Akaitikia hilo.

Nikamwangalia, nami nikasema, “Umekuwa kwa daktari pia, naye akasema ulikuwa na uvimbe maji kwenye ovari.”

Akasema, “Hiyo ni kweli.” Ndipo nikaangalia, nami nikaona msafara wa mazishi, nikasema, “Jiandae kwa ajili ya mauti.”

Naye akasema, “Unamaanisha nini?”

47 Nikasema, “Hutaishi ila kwa muda kidogo tu.” Na katika dakika kumi, huyo mwanamke alikuwa ameketi chini karibu na mumewe, akaanguka kutokana na mshtuko wa moyo, akafa. Na, sasa, kama ningekuwa mponyaji, ningalimponya.

48 Na usiku uo huo, meya wa mji, rafiki yake, akafa, mwanamke mzee, mwenye umri wa miaka sitini, ndipo nikapelekwa mahali alipokuwa, naye akafufuka katika wafu. Mnaona? Ni Mungu, Yeye hufanya tu atakalo.

49 Sasa, kumbukeni, ninyi mnaosoma haya ya Wafanyabiashara Wakristo, walipoweka mle “amewafufua wafu,” kumbukeni, kabla hujaweka hilo hadharani, huna budi kuwa na taarifa zilizoidhinishwa kutoka kwa madaktari, na kadhalika, kwamba hiyo ni kweli. Na kila kitu mnachosoma mle ndani, tuna taarifa zake zilizoidhinishwa.

50 Yu—yule mtoto mchanga aliyekufa kule Mexico, kama mlivyosoma, mtoto huyo alikufa asubuhi hiyo saa tatu, iliidhinishwa na daktari, na ilikuwa ni saa nne usiku huo wakati maskini yule mwanamke Mkatoliki aliyesimama katika ninii, kule chini akipiga mayowe, na kuendelea, ambapo watu thelathini ama arobaini elfu . . . Nami nikamtuma Ndugu Moore huko chini kumwombea huyo mtoto. Nao, mbona, mabawabu thelathini au arobaini wasingeweza kumzuia asiingie mstarini, angekimbilia katikati ya miguu yao na kila kitu akijaribu kupanda kule juu, huku mvua ikinyesha kwa nguvu ilivyoweza kunyesha.

51 Nikaangalia nje na kumwona mtoto mchanga amesimama, ananiangalia akitabasamu, nikasema, “Mleteni hapa.” Mara

nilipoweka mikono juu ya maskini blanketi iliyolowa maji, maskini jamaa huyo akaanza kurusha mateke na kupiga mayowe. Akaruka chini kusema Salamu Maria, nami nikasema, "Hiyo haihitajiki, mpe Mungu sifa," akaenda zake.

52 Na kwa hiyo, ndipo Ndugu Espinoza akaenda kwa madaktari, akamfuatilia kesho yake. Nasi tuna taarifa iliyoidhinishwa na daktari kwamba mtoto huyo alikufa kwa nimonia maradufu asubuhi hiyo saa tatu, na hii ilikuwa yapata saa nne na nusu usiku uliofuata, kwa hiyo, wakati mtoto huyo alipofufuka, taarifa iliyoidhinishwa.

53 Hilo mtaona kuhusu Ufini, ninaye meya wa hilo jiji, kwa muhuri wake mwenyewe, kwamba alikuwako wakati huyo mvulana alipokuwa amelala maiti, amepondwapondwa na motokaa, kisha akafufuka kutoka kwa wafu kwa ono lililoelezewa hapa miaka miwili kabla halijatukia. Mnaona? Kwa hiyo, hizi zote ni taarifa zilizoidhinishwa kwamba ni za kweli.

54 Sasa, mwisho wa uamsho huo alasiri hiyo, ama, mwisho wa mkutano huo, kulikuwa na maskini mvulana mdogo mwenye makengeza aliyefuata. Basi maskini jamaa huyo, angeninii . . . Ningekwambia kile, jinsi wanavyokula, bali ingewachefua, wanachopata kula. Endapo kimejaa mabuu, hiyo ni nyama ya ziada tu, kwa hiyo hawayajali, mnaona, wa—wanajijengea kinga kutoka kwake, kwa hiyo wa—wao wanakula. Na kwa hiyo angeninii . . . damu ilikuwa imejaa kote kwenye maskini tumbo lake.

55 Naye alikuwa ni Mzulu, Mzulu ni mtu mkubwa mno, mwenye nguvu. Anatupa asegai yake, kwa mkono wake, anamfinyilia simba ardhini, nao Washangaani, na wengi wa hao ni jamaa wadogo wanaomwacha simba aruke moja kwa moja kwenye mkuki, waliburuta huu, tunaoita mkuki, wanauita *asegai*.

56 Kwa hiyo, maskini jamaa huyu akija jukwaani, nikasema, "Sasa, kusanyiko linaweza kuona maskini huyu mvulana a—ana makengeza," nikasema, "mtu yeyote anajua hilo." Nikasema, "Sasa, nisingeweza kumponya mtoto huyo, mtu yeyote anajua." Lakini nikasema, "Sasa, kama Roho Mtakatifu angeweza kufunua kilichosababisha hilo, ama jinsi lilivyotukia . . . " Nikamwangalia huyo mvulana mdogo, nami nikasema, "Naam, baba na mama yake kidogo ni adimu kwa Wazulu, mama yake ni mwanamke mwembamba sana, nao ni Wakristo. Katika kibanda wanachoishi, unapoingia, upande wa kulia wa mlango, kuna picha ya Kristo iliyotundikwa ukutani. Naye huyu mtoto alizaliwa akiwa na makengeza." Na yapata yadi mia moja kutoka kwangu, mama na baba wakasimama kutoa ushuhuda kupitia kwa m—mkalimani wa Kizulu, ninao kwenye . . .

57 Na wakati nilipomwangalia huyo mvulana mdogo tena, macho yake yalikuwa sawa tu kama yangu, Nikasema, "Mtu

yeyote anaona ya kwamba huyo jamaa mdogo ameponywa, kwa hiyo mpisheni tu."

58 Kwa hiyo nikaanza kuondoka, katika dakika chache nikasikia fujo huko nyuma jukwaani nikaangalia pande zote, ilikuwa ni maskini daktari Mwingereza, naye maskini daktari huyu alikuwa akiteta juu ya hilo.

59 Na kwa hiyo, Ndugu Ern Baxter. . .Ninajua wengi wenu mnamjua Ndugu Ern Baxter, na ni wangapi waliopata kusikia habari za F. F. Bosworth? Nilisikia kwamba alikuwa. . .Nilisikia huyo alikuwa mmoja wa watu wa mwisho waliofanya uamsho wa Kiungu wa uponyaji hapa katika mji huu, ama, kote humu nchini. Msingeliweza kuwa na walio bora zaidi. F. F. Bosworth, wakati mimi. . .wakati alipokuwa akifa nilimshika mikononi mwangu na kulia, "Baba yangu, baba yangu, magari ya Israeli na wapanda farasi wake!" Alikuwa ni mtu aliyeleta heshima na mamlaka kwa kanisa la Kipentekoste, F. F. Bosworth.

60 Vema, alikuwa jukwaani. Alikuja, a—akasema, "Ninataka kuzungumza naye."

61 Ndipo mtu huyo akasema, "Sasa, wakati Ndugu Branham akiwa chini ya upako, utasababisha ghasia za kijamii hapa, ama chochote kile," maana walikuwa na wanamgambo huko nje kwa vyovyote vile, wakiangalia, maana wana vita vya kikabila.

Na kwa hiyo nikasema, nikageuka, nikasema, "Kwani kuna nini, Daktari?"

Naye akaniangalia, akasema, "Ulijuaje mimi ni daktari?"

Nikasema, "Una udadisi mwingi wa nini?"

Akasema, ndipo wakamruhusu aje, naye akasema, "Bw. Branham, ulimfanyia nini mvulana huyo?"

Nikasema, "Hakuna kitu."

Akasema, "Unajaribu ku—kuingiza mazingaombwe ya aina gani?"

Nikasema, "Unamaanisha nini?"

62 Akasema, "Huyo mvulana, ulimfanyia nini? Je, ulimpumbaza akili mvulana huyo?" Akasema, "Nilimweka jukwaani, papo *hapo*, mimi mwenyewe, naye alikuwa na makengeza, sasa yeye hana makengeza." Kasema, "Kwani ulimpumbaza?"

63 Nikasema, "Kwani Shirika la Madaktari la Uingereza linakupa kibali cha kufanya udaktari, wala hujui zaidi juu ya kupumbaza kuliko hiyo?" Nikasema, "Ikiwa kupumbaza kutanyosha macho ya mtoto, hivi hufikirii ninyi jamaa mnapaswa kuwa mkijizoeza, kidogo, juu ya kupumbaza?" Hiyo ni kweli, naam.

Naye akasema, “Nina shauku ya kujua, Bw. Branham.” Akasema, “Mimi ni Mkristo, nimelelewa katika kanisa la Kianglikana.” Akasema . . .

64 Sasa, yale mayungiyungi ya kala huko, akina dada, mnapaswa kuyaona! Yetu madogo kama *hayo*, baadhi yao yana upana wa inchi kumi na nane, yakikulia mwituni huko jangwani . . . misituni, manjano, na meupe. Kulikuwa na mashada makubwa mno yake yamewekwa kila mahali.

65 Akasema, “Sasa, ninajua kuna Mungu, maana yungiyungi hilo lisingeweza kuishi bila uhai,” akasema, “uhai huo umefichwa mahali fulani katika hilo yungiyungi.” Akasema, “Ninajua kuna Mungu, lakini kwamba yu dhahiri kutosha kuyanyosha macho ya mtoto mwenye makengeza, siwezi kuelewa hilo.”

Nikasema, “Bwana, kamwe sikumgusa mtoto huyo. Hiyo ilikuwa mbele ya wasikilizaji hapa, walimwona mtoto huyo akiwa na makengeza.”

“Kati ya *hapa*,” akasema, “kitu fulani kilitukia kati ya *hapo* na *hapa*.”

Nikasema, “Yesu Kristo alimponya.”

Na kwa hiyo, Bw. Bosworth akamshika mkono, akasema, “Bwana, itakubidi tu kurudi.”

66 Naye akasema, “Ngoja tu kidogo.” Kulikuwa na maikrofoni kubwa ya utando *hapa*, kwa sababu ilikuwa ikipeleka sauti mbali, kwa bloku kadhaa za mji walimokuwa wamekaa, na kadhalika. Akasema, “Hebu kidogo.” Akasema, “Bw. Branham, je, unaniambia ya kwamba Yesu Kristo ni dhahiri sana hivi kwamba anaweza kuyanyosha macho yenye makengeza?”

Nikasema, “Hiyo ni kweli, kwa imani, kama unaamini.”

Akasema, “Basi ninamkubali kama Mwokozi wangu binafsi.”

67 Ndipo nilipoondoka, huko Johannesburg yapata sita . . . yapata—yapata siku kumi baadaye, kulikuwako na yapata watu ishirini au thelathini elfu huko nje wakituaga, naye akaruka juu ya ua akawakwepa walinzi, na kutoka nje mbio, na kunishika shingoni, naye amekuwa mmishenari, na wakati aliponikumbatia shingoni, alianza kunena kwa lugha, huko nje jukwa- . . . huko nje uwanjani. Sasa, yeye ni, bali yeye ni daktari wa tiba kwa daktari wa kimishenari huko nyuma katika nchi kuu za Afrika, usiku wa leo.

68 Mwingine aliyekuja jukwaani . . . Kama mtaniwia radhi kwa kuchukua muda huu wote kwa ajili ya ushuhuda. Wao . . . Mtu mwingine aliyekuja, walimwongoza kama mbwa, alikuwa amefungiwa mnyororo shingoni mwake. Wala nisingeweza kuelezea ili—ilivyokuwa, kwa sababu ni kusanyiko lililochanganyika. Lakini huyo mtu hakuwa amewahi

kuoga maishani mwake, labda alikuwa kwenye umri wake wa miaka ishirini na kitu, alitembea kwa mikono na miguu yake amefungwa mnyororo shingoni mwake, hata hakuwa na akili timamu.

69 Na kwa hiyo wakampandisha juu. Nami nikasema, "Maskini mwanadamu huyo! Kama mtu yeyote angeweza kumsaidia mtu huyo wala asingefanya hivyo, hata hawastahili kuishi wenyewe." Nikasema, "Nisingeweza kumsaidia zaidi, kuliko... Kama Roho Mtakatifu angeniambia kilichompata," nikasema, "Ni—ningeweza kufanya hivyo kwa karama ya Kiungu. Lakini kama ataamini," nikasema, "basi nitamwombea."

70 Na kwa hiyo, nikaanza kumwangalia, nikasema, "Alizaliwa hivyo." Basi ikatokea kwamba wazazi wake hawakuwa wameketi mbali sana. Nami nikasema, "Lakini sasa, kwa kuwa nimevutia usikivu wake, yeye anawazia juu ya ndugu yake. Ndugu yake alikuwa akipanda," Nikasema, "ama juu ya mbuzi wa manjano, au mbwa wa manjano, ndipo...akaumiza goti lake, naye anatembea kwa mikongojo miwili." Nikasema, "Yeye ni mdogo na mwembamba sana kuliko mtu huyu." Lakini nikasema, "Popote alipo ndugu yake, BWANA ASEMA HIVI, ameponywa." Nikasema, "Haimbidi kutembea kwa marungu yake tena."

71 Ndipo yapata umbali wa jengo moja la mji nikasikia mayowe, naye huyu hapa anakuja, akiruka kwa nguvu alivyoweza, ameshika marungu mikononi mwake. Naye akapata...Akaponywa. Vema, basi ilituchukua kama dakika ishirini kuwatuliza.

72 Katika wakati huo, niliangalia, nami nikaona ono juu yake, mtu huyo alikuwa amesimama mzima, nikawaza, "Loo, jamani! Huu hapa wakati wa kuwashika wasikilizaji wangu sasa." Nami nikasema, "Kama Mungu atamfanya maskini mtu huyu kiwete kuwa mzima, ni wangapi wenu ninyi watu watamkubali Yesu kama Mwokozi wenu?" Na kadiri ungeweza kuona, mikono myeusi imeinuliwa namna *hiyo*.

73 Nilijua litatukia, maana tayari nilikuwa nimeliona lile ono, mnaona. Unapoona hilo, hayo yote yamekwisha basi, hakuna wa kutosha, hakuna pepo wa kutosha kutoka kuzimu wangeweza kukomesha hilo basi maana tayari, ni kazi iliyomalizika, jambo pekee, linangojea tu kutukia. Hivyo ndivyo hasa Bwana wetu alivyosema. Hivyo ndivyo mtu yeyote wa Biblia...Yesu alisema, "Sifanyi neno, mpaka nitakapomwona Baba akilitenda kwanza." Mnaona? Kwa hiyo ni sawa kabisa.

Kwa hiyo nikamwangalia huyo mtu, nilijua atapona, kwa hiyo nikasema, "Kwenu ninyi Waislamu huko nje." Mikono yao ikainuliwa.

74 Sasa, nikasema, "Simama kwa miguu yako, Yesu Kristo anakuponya." Naye akajaribu...Unajua wanawafanyia watalii

vitimbi sana. Wao—wao walijaribu...Alidhani alikuwa akicheza dansi ya kikabila, alikuwa akichukua mikono yake namna *hii*, maskini mtu hata hana akili timamu. Nami nikasema, "Sikumaanisha hivyo, sikumaanisha hivyo."

Naye mkalimani alikuwa akijaribu kumwambia. Nikasema, "Simama."

Naye alikuwa akifanya, "Ah blurr la blurr blurr," kana kwamba alikuwa akicheza, mwajua, akijaribu kufanya, kwa mikono na miguu yake, hana nguo, kitambaa tu.

75 Ndipo nikaushika huo mnyororo, nikasema, "Simama, Yesu Kristo anakuponya." Ndipo alipopata kile...akasimama kwa miguu yake kwa mara ya kwanza maishani. Hapo, machozi yakitiririka kwenye tumbo lake jeusi, akitema mate namna *hiyo*.

76 Ndipo nikawaona wenyeji elfu thelathini wanaovaa blanketi wakimjia Yesu Kristo katika wito mmoja wa madhabahuni. Nikasema, "Ni wangapi wenu watampokea Kristo kama Mwokozi binafsi?" Ndipo elfu thelathini wakasimama kwa miguu yao. Nami nikasema...

77 Ndugu Baxter akasema, "Ndugu Branham, nafikiri walimaanisha uponyaji wa kimwili." Nikasema, "Mimi—mimi," lipitishe kwa wakalimani tena, Nikasema, "Sikumaanisha uponyaji wa kimwili, nilimaanisha ya kwamba una... unamkubali Kristo kama Mwokozi wako, Mwana wa Mungu, basi iwapo ninyi ni waaminifu, zivunjeni sanamu zenu ardhini." Na ilionekana dhoruba ya mavumbi, kana kwamba bomu la atomiki lilikuwa limelipuliwa, ndipo uyoga wa mavumbi ukapaa juu namna *hiyo*.

78 Ndipo kesho yake asubuhi, Sidney Smith akanipigia simu, akasema, "Ndugu Branham," Jumatatu asubuhi, akasema, "hujapata kuona kitu kama hiki!" Kasema, "Kuwa...Nenda kwenye dirisha la hoteli yako linaloelekea baharini, uwatazame wakishuka barabarani."

79 Ndipo nikaangalia, huku wakishuka mtaani, na kulikuwa na malori saba ya mizigo...Sasa, ninyi mliomjua F. F. Bosworth, mnajua hatoi hesabu ya kiinjilisti. Nilifanya maombi ya kusanyiko, kulikuwa na watu wanne jukwaani, nikafanya maombi ya kusanyiko, naye F. F. Bosworth akakadiria miujiza elfu ishirini na tano ilifanyika kwa wakati mmoja. Mbona, ilikuwa—ilikuwa kubwa mara kumi kuliko Pentekoste!

80 Na sasa, na hapa, wanashuka kuja barabarani kesho yake asubuhi, saba ya hayo malori makubwa ya Kiafrika, jamani, marefu kuliko malori yetu ya trela hapa, yamelundikwa tu maskini...ya vitu walivyokuwa wamevibeba, na marungu, na machela, na mikokoteni, na vitu walivyowasukumia. Nao hawa hapa wakija nyuma, walikuwa wameketi ndani yake siku iliyotangulia, na kesho yake wanatembea barabarani, wakiimba, "Amini tu, mambo yote yanawezekana, amini tu."

81 Nimeusikia mara nyingi, na umeisisimua nafsi yangu kila ninapousikia, kwa sababu umekuwa wimbo wangu mkuu kwa miaka mingi, lakini kamwe haukugusa moyo wangu namna hiyo kusikia thelathini. . .maelfu hayo yote mara maelfu ya wenyeji wakishuka kuja mtaani hawako vitani tena. Nina sehemu moja kutoka kwenye gazeti la Durban, lililosema katika muda wa miezi mitatu, ninasahau ni bunduki ngapi na mashehena ya vitu walivyokuwa wameiba, ambavyo vilikuwa, wakivirejesha, walikuwa wamemalizana na dhambi.

82 Hebu niseme jambo lingine hapa, tunapaswa kuwa katika ustaarabu, hao wanawake, wakisimama pale, hao wanawake, mmoja alijifungua mtoto, ameketi si futi ishirini kutoka kwangu. Kamwe hakuwa na daktari, alimwokota tu maskini jamaa huyo mdogo. Mama mwingine karibu naye alikuwa nayo, akamzaa mtoto, akampa maskini kichemsha matako. Kisha akamwinua kwenye titi lake akaanza kumnyonyesha huyo mtoto, na akaendelea kumpembeza mtoto huyo mchanga, huku ananisikiliza nikihubiri. Washamba tu wawezavyo kuwa! Lakini mnajua nini? Mara walipompokea Yesu Kristo kama Mwokozi binafsi, wamesimama pale pasipo na kitu ila kitambaa kidogo karibu *hivyo* kikining'inia mbele yao namna *hiyo*, walipoondoka kwenye uwanja huo, walikunja mikono yao waondoke mbele ya wanaume, kutafuta nguo za kuvaa.

83 Sasa, ni kwa nini tunajiita Wakristo, huku tunavua nguo nyingi zaidi kila mwaka? Sasa, siwezi kuelewa hilo, wakati kafiri kabisa anapompokea Kristo, wanaanza. . .wanatambua ya kwamba wako uchi, na kukunja mikono yao, hao akina mama, na kuondoka. Mungu isaidie Marekani! Katika—katikati ya moyo wangu, ninahisi machozi yakidondoka, "Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi nimetaka kuwakusanya pamoja, kama kuku awakusanyavyo vifaranga wake!" Lakini hebu niwaonye, saa imekaribia.

84 Mtu fulani ameacha noti ya dola kumi hapa, sidhani ilikuwa ni kwa ajili yangu, kwa hiyo kama ndivyo, uh, pale, labda ilikuwa kwenye matoleo, ama chochote kile, ni mali ya mtu fulani. Natumaini sininii. . .nitaiweka moja kwa moja chini ya Biblia hii, yeyote yule, aliyewekewa hapo.

85 Sasa, ninasikitika kuwaweka muda mrefu, lakini mimi—mimi—mimi, mara kwa mara, ninapenda tu kushuhudia. Nitajaribu nisikae zaidi ya saa nne usiku wa leo, katika jambo hili, ikiwa naweza kuizuia. Nami ninaninii. . .na kama nikipitisha hizo, mtu fulani avute koti langu, kama nikininii. . . Simaanishi kufanya mzaha, bali nilisema tu hilo makusudi, hebu tujiandae sasa.

86 Na kabla hatujalikaribia Neno, hebu na tumkaribie Mwandishi. Ni wangapi wanaomjua Booth-Clibborn, William Booth-Clibborn? Loo, yeye ni msemaji hodari! Huhubiri katika

lugha saba mbalimbali, naye ni rafiki msiri wangu. Aliandika wimbo ninaoupenda sana, *Alishuka Kutoka Utukufuni Mwake*, naye ni . . . loo, aliandika, *Tazama Bwana Arusi Yuaja*, na nyingi za nyimbo hizo. Yeye ni Mwingereza, bali yuko Oregon sasa. Yeye ni mtu mzuri, mtu mzuri sana, lakini, ni ninii sana . . . Loo, jamani, anajua . . . Anaweza kuhubiri Biblia katika Kiyunani, kuihubiri katika yoyote atakayo, a—anahubiri katika lugha saba.

87 Kwa hiyo siku moja mimi na yeye tulikuwa huko Shreveport pamoja na Ndugu Moore, nasi tulikuwa tukijadili jambo fulani, nami nilikuwa upande wa pili wa huo mjadala. Nami nikamwambia Ndugu Booth *jambo lingine* kulihusu, naye akasema, "Lakini sikiliza hapa, ewe jamaa mdogo," akasema, "huijui tu Biblia yako."

88 Nikasema, "Huenda hilo likawa ni kweli, Ndugu Booth, bali ninamjua Mwandishi wake vizuri sana."

Akasema, "Sasa, hilo si linapendeza?" Kasema, "Jack, huna budi kumpenda, kwa vyovyote vile."

89 Kwa hiyo, afadhali nimjue Mwandishi, kuliko kukijua Kitabu Chake, kwa sababu Yeye atakifunua hicho Kitabu kama tunamjua Mwandishi wake. Kwa hiyo, kabla hatujaingia kwenye hiki Kitabu, hebu na tuzungumze na Mwandishi wake, huku vichwa vyetu vimeinamishwa, tafadhalini.

90 Mungu mkuu mwenye nguvu zote, wa Milele, asiye na kikomo, tunakikaribia kiti Chako cha rehema kwa unyenyekevu, kwa sababu tumealikwa kuja na Bwana Yesu, kwa kusema, "Mkimwomba Baba lolote katika Jina Langu, nitalifanya." Ndipo tunakuja na hakikisho lililobarikiwa la kujua ya kwamba tutapata kile tunachoomba, hakuna hata kivuli kimoja cha shaka mioyoni mwetu. Kama kipo, tusamehe, Bwana, kwa kuwa ni dhambi kutokuliamini Neno la Mungu na ahadi Yake.

91 Tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atakuja pamoja nasi usiku wa leo, ataingia katika maneno haya machache yaliyopangwa kutoka kwenye muktadha wa kifungu hiki ambacho nimechora, usiku wa leo, kuwazungumzia hawa, walionunuliwa kwa Damu Yako.

92 Nami ninajua, Baba, jinsi ningejisikia kama ningeshikilia katika bilauri, usiku wa leo, matone mawili ya Damu halisi ya Mwanao wa thamani. Jinsi ningeikumbatia moyoni mwangu, ingenibidi kuishikilia kando kuzuia machozi yangu yasidondokee ndani yake, kujua ya kwamba hiyo Damu ndiyo iliyoniokoa, iliyoniponya! Kwa Damu hiyo, nilifanyika mwana wa Mungu kwa neema Yake. Jinsi ningeithamini, na kuwa mwangalifu kwamba ni—nitaweka mguu wangu sawasawa, nisingetaka kujikwaa niimwage bure!

93 Lakini, Bwana, usiku wa leo, machoni Pako Mwenyewe, umeweka mikononi mwangu hazina kubwa Kwako kuliko hiyo

Damu. Kwa kuwa Wewe umeweka mikononi mwangu, usiku wa leo, kilichonunuliwa kwa Damu hiyo, kwa kuwa, kwa kweli, Wewe uliwawazia watu Wako zaidi ya vile ulivyoiwazia Damu Yako Mwenyewe, kwa sababu ulimwaga Damu Yako kwa ajili yao.

94 Basi yanipasa kuwaendea namna gani, Bwana? Kwa moyo mnyofu, mwaminifu, uliojitolea kabisa pamoja na hakikisho, tukimngojea Roho Mtakatifu kwa ajili ya upako, kwamba maneno ninayosema yatanikabili usoni mwangu kwenye ile Siku ya Hukumu, wakati watoto Wako watakaposimama kule. Mungu uturehemu.

95 Ninaomba ya kwamba umtakase mnenaji na msikiaji. Yatie mafuta haya maneno yapate kuanguka ndani ya mioyo ya watu, yapate kuzaa mara mia, hili ndilo kusudi letu, lengo letu ni kuona Ufalme wa Mungu ukiendelea. Mungu, tunaamini ni mapenzi Yako, kwa hiyo na itimie kwamba tutamwona Yesu Kristo akiwaokoa wenye dhambi, kuwarudisha nyumbani kwenye ushirika waliorudi nyuma, na kuwaponya wagonjwa kwa imani katika Jina Lake. Amina.

96 Sasa, tukiweka kando mawazo yetu yote, mambo madogo ambayo huenda tuliyawazia ama kuyasema, hebu na tuyaendee haya katika utaratibu wa Kiungu. Ninapenda kulisoma Neno, kwa kuwa neno langu litashindwa, mimi ni mwanadamu, lakini ninasoma Neno Lake, ndipo kama hakuna kitu kingine, hampati kitu kingine, mtapata *kitu* nitakapolisoma Neno.

97 Katika Mathayo 12:42, tunasoma Maneno haya:

> Na *malkia wa kusini atasimama...hukumu pamoja na watu wa kizazi hiki, naye atawahukumu kuwa wamekosa: kwa sababu yeye alikuja kutoka pande za mwisho za dunia ili asikie hekima ya Sulemani; na, tazama, hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani.*

98 Ningetaka kuchukua hilo kama somo: *Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa.*

99 Sasa, Yesu alikuwa akikemea kizazi Chake kwa kutoiamini huduma Yake. Jinsi Mungu alivyoifanya dhahiri, na, hata hivyo, hawakuiamini. Nao walikuwa wamemjia wakitafuta ishara, Naye angewapa ishara. Nao walijua, na walifundishwa vizuri zaidi, wasijaribu kamwe kuamini theolojia ya moja kwa moja, kwa sababu zimezidi...zipo nyingi za hizo. Lakini Mungu daima alijithibitisha Mwenyewe kwa ishara inayothibitisha theolojia.

100 Sasa, kama kuna wanafunzi wa Biblia hapa, ambapo niko katika chuo cha Biblia, nami ninazungumza mbele ya wahudumu werevu, na wanafunzi, na mtu yeyote anajua ya kwamba katika Agano la Kale walikuwa na torati, hiyo ilikuwa ni zile Amri Kumi, na halafu walikuwa na kile walichokiita Urimu na Thumimu. Hiyo Urimu na Thumimu ilikuwa ni

mkusanyiko wa Nuru zilizoakisi kutoka kwenye kile kifuko cha kifuani ambacho Haruni alivaa, cha yale mawe kumi na mawili, ambayo yaliwakilisha yale makabila kumi na mawili ya Israeli, mawe yao ya kuzaliwa.

101 Sasa, wakati nabii alipotabiri, ama mwotaji alipoota ndoto, haidhuru ilionekana halisi jinsi gani, theolojia huenda ikawa ni kamilifu, kweli kabisa, lakini kabla hawajaweza kuikubali kwamba imetoka kwa Bwana, waliwapeleka kwenye Urimu na Thumimu, na kumwacha nabii huyu atoe unabii akiikabili hiyo Urimu na Thumimu, ama mwotaji asimulie ndoto yake. Na kama Urimu na Thumimu hazikusogea kamwe, ilikuwa ni ya uongo, lakini iwapo hiyo Urimu na Thumimu iliingia katika mambo ya kimbinguni na kusababisha mkusanyiko wa Nuru, zikitoka kwake kimbinguni, kama ishara, basi huyo nabii alikuwa sahihi, hilo lilikuwa ndilo thibitisho.

102 Kumbukeni Sauli, jinsi alivyosema hata Urimu haingemjibu, na kadhalika? Mnaona? Hiyo ilikuwa ndiyo njia yao ya kulijua.

103 Sasa, siku hizi, baada ya ukuhani huo wa Haruni kukoma, Mungu anayo njia nyingine, Urimu na Thumimu nyingine, hiyo ni Biblia. Kama mtu huyo akihubiri jambo lolote ambalo ni kinyume, wala halipatikani katika Neno la Mungu, basi nitaachana nalo. Lakini kama akihubiri yaliyo katika Neno, kisha Mungu arudi na kuthibitisha kwa ishara ya Urimu kwamba ni kweli, basi huyo ni Mungu akishuhudia ya kwamba hilo ni kweli, kutokuamini hilo ni kuangamia.

104 Yesu, Wayahudi walifundishwa kuamini ya kwamba wangekuwa na Masihi, nao waliambiwa ya kwamba Masihi huyu angekuwa ni Nabii, nao walikuwa wameambiwa ya kwamba Yeye angefanya ishara ya nabii. Sasa, Israeli walikuwa na njia ya kumjaribu nabii, kwa kuwa kama nabii alitabiri, na kwamba yale aliyosema hayakutimia, basi yeye hakuwa nabii, achana naye, lakini kama ilitimia, basi msikieni, kwa sababu Mungu alikuwa amemtuma.

105 Sasa, basi Masihi huyu alikuwa ndiye Mkuu na Mungu wa manabii *wote*, Yeye alikuwa juu yao wote. Mungu alikuwa na nabii mmoja tu mkuu katika kizazi chochote, kamwe hapajakuwapo na wawili uwanjani kwa wakati mmoja. Eliya na Elisha walitembea pamoja kwa karibu, bali kamwe hakuwa nabii kabisa mpaka vazi la Eliya lilipomshukia, hiyo ni kweli. Mnaona? Walikuwa na manabii wadogo, na kadhalika, lakini yeye, nabii ni mtu anayezaliwa, na kuchaguliwa tangu zamani, na kukusudiwa tangu awali kwa ajili ya kizazi hicho, Biblia inafundisha jambo hilo, hiyo ni kweli. Kwa kujua kwa Mungu tangu zamani Yeye alimweka mtu fulani kwa ajili ya jambo hilo.

106 Sasa, basi wakati Yesu alipokuja na kutimiza Maneno yote ambayo . . . Yeye alidhaniwa kuwa ndiye Nabii *yule*. Hivi hamjui, walimwuliza . . . ?

“Watu husema mimi ni nani? Wanasema nini?”

“Je, Wewe ndiwe yule Nabii?” wakasema.

“Wewe umesema.” Mnaona?

107 Ama, “Tunamtafuta Nabii.” Yule mwanamke kisimani, kama tulivyozungumzia hivi majuzi usiku, alisema, “Tunajua ya kwamba ajapo Masihi, Yeye atakuwa ndiye yule Nabii, Yeye ni yule Mtiwa mafuta, Yeye atatuonyesha ishara ya Masihi.”

Yesu alisema, “Mimi ninayesema nawe, Ndiye.”

Akaingia mjini, na kuwaambia hao watu, “Haimkini Huyu kuwa ndiye Masihi? Aliniambia mambo ambayo nimefanya.” Nao hao watu wakamwamini.

108 Sasa, mnakumbuka, Yeye kamwe hakumponya mgonjwa yeyote, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu, Alijua ya kwamba Filipo alikuwa akishuka kuja kuwaponya wagonjwa baada ya Pentekoste. Yeye alizungumza nao tu, hakufanya mwujiza mmoja zaidi, bali hilo lilithibitisha ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi, kwa sababu alijua siri ya moyo.

109 Sasa, ni wangapi wanaoamini, katika kusanyiko hili, pamoja nanyi Wamethodisti, Wabaptisti, na Wapentekoste, na chochote ulicho, ni wangapi wenu wanaoamini ya kwamba Biblia ni ya kweli katika Yohana Mtakatifu 1, ambapo inasema, “Hapo mwanzo alikuwako Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu”? Hiyo ni kweli? Huyo alikuwa ni Kristo.

110 Ni wangapi wanaoamini basi Waebrania 4, ambapo ilisema, “Neno la Mungu. . . ” Ambalo ni Kristo, hiyo ni kweli? Yeye ni Neno lililo hai. “Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, na hata Mtambuzi wa mawazo ya moyo.” Turudi kwenye Neno tena, nalo Neno liko pamoja nasi.

111 Sasa, Neno la Bwana linakujaje? Neno lilikuja kwa, Neno la Mungu lilimjia nabii. Hawakuhoji kamwe, kwa sababu alikuwa na Neno la Bwana, kwa sababu yale aliyosema yalitimia, kwa hiyo ilikuwa ni Neno la Bwana.

112 Naye Yesu alikuja akitenda hayo, nao wakamwita mpiga ramli, Beelzebuli, ibilisi. Na kuita kazi ya Mungu pepo mchafu, Yeye alisema, ilikuwa ni kumkufuru Roho Mtakatifu wala halingesamehewa katika ulimwengu huu, wala ulimwengu ujao.

113 Si ajabu alikuwa akiwakemea, akiwaambia. Wao walisema, “Tunatafuta ishara,” na baada ya Yeye kuthibitisha ishara yenyewe ya Masihi. Nao walikuwa wamezama sana katika theolojia yao, hata hawakutaka kuiona. Hawakutaka tu kuiona, hivyo tu, ilikuwa dhahiri mbele ya uso wao.

114 Sasa, mtu yeyote aliye na. . .ambaye anajua, aliye na akili timamu, na atajua Biblia, anajua ya kwamba Yesu kamwe hakuja kinyume cha Maandiko, Alikuja na Maandiko, bali

alikuja kinyume cha theolojia yao. Na hivyo ndivyo Roho Mtakatifu amekuja katika siku za mwisho, amekuja sawasawa kabisa na Maandiko, bali kinyume cha theolojia ya watu. Hilo ni dhahiri? Mnaona? Hiyo, Yeye huja hivyo.

115 Sasa, Yeye alikuwa akiwakemea kwa sababu hawakuamini ishara Yake ya Masihi, nao walikuwa wameiita pepo mchafu. Soma tu yanayofuata . . . mlango uliosalia . . . mwanzo wa mlango huo, uone kilichokuwa kimetukia.

116 Wakati alipomwambia Nathanaeli, pale, siku hiyo, kasema, “Nilikuona, kabla hujawa chini ya . . . ulipokuwa chini ya mtini, nilikuona.” Nathanaeli akiwa mtu aliyekusudiwa Uzima wa Milele, alisema, “Rabi, Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.”

117 Akasema, “Heri wewe.” Mnaona? “Kwa kuwa nilikwambia jambo hili, uliamini? Unaweza kuona mambo makuu kuliko haya.” Mnaona, yeye yuko tayari basi kupiga hatua kuingia katika nyanja nyingine, mara tu yeye . . . Angeona mambo makuu zaidi, kasema, “Utaweza kuwaona Malaika wakishuka, na kupaa, juu ya Mwana wa Adamu,” sasa, maana alikuwa anakuja katika viwango vya juu zaidi.

118 Kama wewe ambaye ndio kwanza umkubali Kristo kwa kuhesabiwa haki, mkubali Yeye kwa utakaso, na uyasafishe maisha yako, ungali unavuta sigara, angalia kinachotukia, ni tofauti jinsi gani, unaangalia nyuma kwenye kuhesabiwa haki. Wewe, ambaye umesimama tu umehesabiwa haki, kamwe hukupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu, ingia kwenye mazingira hayo, kisha uangalie tena mengine yote. Unaona? Endelea tu kutembea, mpaka baada ya kitambo kidogo utakuwa mwepesi sana, unaweza tu kutembea uingie kwenye Unyakuo. Panda tu juu moja kwa moja. Unaona?

119 Tulizoea kuimba wimbo wa kale, “Kila siku hunifikisha raundi moja juu zaidi, juu zaidi.” Unaona? Hivyo—hivyo ndivyo inavyotupaswa kufanya, kamwe usiwashe moto ule ule uwanjani usiku wa pili, endelea tu kupanda juu zaidi, juu zaidi.

120 Nilikuwa Phoenix siku chache zilizopita, nao walikuwa wakiimba wimbo mdogo, “Ninapanda juu, juu, juu.” Nami nikasema, “Alipanda juu hata akafika kwenye ile Njia ya Kilimia Cheupe,” huko ndiko tunakopaswa kufika. “Ndipo basi akapata Ufanisi mkubwa, wakati alipofika kwenye ile Njia ya Kilimia Cheupe.” Kwa hiyo hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya.

121 Lakini Yesu akitenda, na kuwaonyesha watu Wake Mwenyewe, hasa kulingana na Maandiko, Naye akakasirishwa nao, Nalo lilisema, “Asingeweza kufanya miujiza mingi kwa sababu ya kutokuamini kwao.” Sasa, wanapomwita Roho Mtakatifu yeye yule katika siku hizi udanganyifu, telepathia ya kiakili, unawezaje kutarajia uamsho? Unawezaje kutarajia, wakati Yesu alisema dhahiri, nao manabii wakatabiri wakati

wa jioni mambo haya yangetukia? Laiti tungalikuwa na mwezi mzima wa kukaa hapa na kulifundisha, mpate kuona, kwa thibitisho lisiloweza kukosea, kwamba ndivyo ilivyo.

122 Ndipo basi wakati Marekani inapoliangalia, wanalifanyia mzaha, mtakatifu anayejibingirisha, mpiga ramli, mtaalamu wa telepathia ya kiakili. Mtu yeyote ambaye angeita upambanuzi wa roho telepathia ya kiakili, mtu huyo ana kichaa. Yeye hajui hatua ya kwanza ya telepathia ya akili, kwa sababu ni saikolojia inathibitisha kwamba hajui anachozungumzia. Inaonyesha kutokujua kwake mwenyewe kwa huduma anayodai ipo. Hata hajui hatua ya kwanza ya saikolojia, kama akiita upambanuzi wa roho *saikolojia*.

123 Watu wanalipata. . .Hawana budi kujibia jambo fulani, na wanapofanya hivyo, badala ya kuomba na kumwomba Mungu alifunue, wanatoa tu maoni yao wenyewe, hayo ni maoni yao kama ilivyo kwenye bustani ya Edeni, majani ya mtini yalikuwa ndiyo bora zaidi, kwa hiyo wanalikubali namna hiyo, "Kanisa langu haliliamini, na hilo latosha." Ni yale Mungu aliyosema, si yale theolojia yenu iliyosema, ni yale Biblia iliyosema juu yake. Hiyo ndiyo hali ambayo Yesu alilipata kanisa. Kwa hiyo tunatambua. . .

124 Na sasa, sitawaweka kama nilivyofanya jana usiku, kama ningeweza kusaidia. Enyi marafiki, mimi hunena tu kwa uvuvio, ninaweza tu kusema kama Yeye asemavyo niseme, na hivyo ndivyo inavyonichukua muda mrefu, wakati mwingine.

125 Lakini na—nawatakeni mwone, ya kwamba Mungu, katika vizazi vyote, kote katika Biblia, Daima amekuwa na wakati Wake ambapo alituma ishara Zake, maajabu, na karama miongoni mwa watu, na, ili kwamba katika ule ufufuo mkuu wa kiama Yeye aweze kuwa mwenye *haki*. Kwa kuwa Yeye anaweza kumsimamisha huyu mtu hapa, usithubutu kulikanusha basi, "Kwa kuwa huyu hapa amesimama mtu ambaye Yeye alisema nawe kupitia kwake, nawe huna udhuru," yale aliyosema kuhusu malkia pale, mnajua.

126 Sasa, na wakati wowote ambapo Mungu aliwahi kutuma karama kwa ulimwengu, nao watu wakaipokea, walifanyika. . . ulikuwa ni wakati wa ufanisi sana kwao, lakini walipoikataa, waliingia katika machafuko, na maafa, na kuingia katika adhabu. Sasa, ninyi wanahistoria wa Biblia, ama, semeni tu ni lini wakati mmoja ambapo waliwahi kukataa karama za Mungu na ishara Zake, nao wakapata ufanisi.

127 Wakati mmoja, walipokuwa wakienda vitani, Yeye alinena, Mungu alinena nao, kasema, "Kama mkitaka kufanikiwa, msiwadhuru manabii Wangu, waaminini manabii Wangu, mkitaka kufanikiwa." Vema sasa, tunajua ya kwamba kama Marekani hii ingeikubali Karama ya Mungu iliyotumiwa. . .

128 Ambapo kutoka Marekani wametoka wainjilisti na wamishenari walioanzisha uamsho wa uponyaji, ulimwenguni kote. Kama vile yule Malaika wa Bwana, miaka thelathini na mmoja iliyopita, alivyonena kule chini mtoni wakati ile Nuru, Nguzo ya Moto iliponing'inia pale, nayo magazeti yakaiandika, *Nuru ya Ajabu Ikitokea Juu ya Mhudumu wa Kibaptisti Wa Mahali Hapo*, mvulana, wakati nikibatiza watu mia tano kwenye Mto Ohio, Naye akasema, "Kama vile Yohana Mbatizaji alivyotumwa kutangulia kule Kuja mara ya kwanza kwa Kristo, Ujumbe huu utakutangulia kwa pili." Sisi hapa. Je, umefanya hivyo? Mnaona? Kutoka hapo ukawachochea akina Oral Roberts, Tommy Hicks, Osborn, na kadhalika, wakazunguka na kuzunguka ulimwengu. Mnaona? Umefanya hivyo.

129 Angalieni, sasa, kama Marekani ingepokea Karama ya Mungu, ungekuwa ni wakati wa ufanisi mkuu sana kwetu, kama makanisa yote ya Marekani yangeikubali Karama ya Mungu. Karama ya Mungu kwa Kanisa ni nini? Roho Mtakatifu. Vipi kama Wamarekani wote waliomwamini Kristo wangempokea Roho Mtakatifu? Isingewabidi kushangaa ni nani atakayekuwa kwenye sputniki, ama ni nani atakayekuwa kwenye ule mtambo wa maili mia moja, themanini mzunguko, Kanisa hilo lingekuwa Utukufuni kabla hawajaweza kuanzisha sputniki. Hiyo ni kweli.

130 Wala huna haja kuwa na wasiwasi kuhusu. . .Sasa, wanaogopa sana. Mbona, kama wa—wao. . .tungelipokea karama ya Mungu kwetu, mbona, isingetubidi kujaribu kuchimba mashimo kujificha kutokana na bomu la atomiki, na kuweka matangazo haya yote ya habari ya kujenga kimbilio la kuendea.

131 Ninataka kuwaulizeni jambo fulani. Wanadai ya kwamba bomu hili jipya la haidrojeni, na hilo ndilo tu tunalojua habari zake, hatujui zile walizoficha, lakini wanaweza kusimama huko Moscow, Urusi, na kutega bomu kwa nyota kuelekea papa hapa kwenye jengo hili, na kulidhibiti kwa rada, nao wameyaelekeza kwenye kila taifa kuu, na kila jiji kuu ulimwenguni, kuvuta tu kamba moja, nalo hilo linarushwa. Mtu fulani atakunywa vodka kupita kiasi siku moja, na hakutakuwa na lingine.

132 Na kila taifa linalosimama. . .Tuna kitu kile kile. Na moja ya hayo mabomu litaingia kwenye skrini ya rada ya mtu fulani moja ya siku hizi, nalo hilo limerushwa. Na hilo lingeweza kutukia kabla ya asubuhi, ila kabla jambo hilo halijatukia, Kanisa litapaa juu. Hiyo ni kweli. Kwa hiyo kama hayo yamekaribia hivyo, Kuja kwa Kristo kumekaribia vipi? Hili halina budi kuondoka kabla hilo halijatukia. Siamini Kanisa litapitia kwenye ile Dhiki, siamini kuna Maandiko ya kuliunga mkono. Mimi. . .Sasa, kama mimi natofautiana, ninyi nyote tupeni hilo nje kama mfupa kutoka kwa kuku, nilisema, ama mbegu kutoka kwa. . .Mnaona?

133 Ila kumbukeni, hapakuwapo na tone la mvua lililoshuka mpaka Nuhu alipoingia kwenye safina, hakukuwako na Moto ulioshuka hata kidogo mpaka Sodoma, uh, Lutu alipotoka Sodoma, Yesu alisema, "Ilivyokuwa katika siku hizo, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa Adamu."

134 Kanisa, tayari, ni, hailibidi kuhukumiwa, tayari limekwisha kuhukumiwa, kwa kuwa lilimhukumu Kristo, naye Kristo alistahimili hukumu Yake. Tunapokuwa ndani Yake, tuko huru na hukumu. Mungu akikuhukumu, basi Yeye hana haki, Kristo alichukua hukumu yetu kwa ajili yetu. "Na kwa Roho mmoja tumebatizwa kuwa Mwili huo. Yeye aniaminiye Mimi yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni," Yohana Mtakatifu 5:24. "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa Milele, wala hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Amina. Hiyo ndiyo Injili. Loo, jinsi tunavyopaswa kuwa na furaha tukiangalia tu na kungojea wakati huo mtukufu! Sasa, lakini Marekani inaihukumu, inaitupa nje, afadhali wawe na theolojia yao.

135 Sasa, Yesu alirejea hapa kwa Sulemani, lakini kabla hajafanya hivyo, kuna mtu mmoja, hapa, ambaye ningetaka kuzungumza habari zake kwa dakika moja tu, na huyo ni yule jamaa, Yona. Watu wengi sana wanamkataa Yona, wanasema, "Loo, yeye ni Yona." Lakini Yona kamwe hakutoka nje ya mapenzi ya Mungu. Nabii anawezaje kutoka nje ya mapenzi ya Mungu? Yeye alikuwa nabii wa Mungu, angewezaje? Nilikuwa nikisoma kitabu hapa si muda mrefu uliopita, juu ya jambo fulani lake. Huenda kilikuwa ni hadithi ya kubuni, huenda ilikuwa ni kweli.

136 Lakini Yona alichukua...Mungu alimwambia aende Tarshishi. Eliya alimwambia Elisha akae huko Gileadi, pia, lakini akaendelea mbele. Mnaona? Lakini inatubidi kuangalia, Mungu huwaongoza watoto Wake, nazo nyayo za wenye haki huongozwa na Bwana, wanaongozwa na Roho Mtakatifu. Wakati mwingine unafikiri unakosea, lakini kama Roho anakuongoza, nenda ukafanye hivyo haidhuru. Roho Mtakatifu akiwaambia baadhi yenu watu mlio kwenye viti vya magurudumu, "Simama uanze kutembea," tembea kwa vyovyote vile.

"Nitatembeaje?"

Hiyo si kazi yako, sikiliza tu yale Roho asemayo. Akikwambia uje madhabahuni, ukatubu, fanya hivyo.

"Jirani yangu, mchungaji wangu..."

137 Sijali anachosema, Kile Roho Mtakatifu anachosema, nenda ukafanye, "Wana wa Miungu wanaongozwa na Roho wa Mungu." Sasa, mara nyingi nimeenda mijini, nilifikiri nilikosea, bali nikaendelea tu kupigana, baada ya kitambo kidogo, halikuwa ni kosa.

138 Yona alipaswa kwenda Ninawi. Ninawi ilikuwa karibu ukubwa wa mji wa St. Louis huku nje, maelfu ya watu, nao walimwacha Mungu na kuanza kuabudu sanamu. Nasi tunajua hadithi hiyo, ya kwamba Yona alipaswa kwenda Ninawi, lakini akapanda meli kwenda Tarshishi. Kwa hiyo kama angalienda Ninawi, hiyo hadithi isingeandikwa kama ilivyoandikwa.

139 Kwa hiyo alikuwa akienda zake Tarshishi, nayo hiyo bahari kuu ikaanza kunguruma na kupiga makelele. Na—naye Yona, mtu mwema, mwaminifu, akawaambia ilikuwa ni dhambi yake, nao wakamfunga mikono na miguu na kumtupa nje baharini, naye Mungu alikuwa na samaki mkubwa pale wa kummeza. Mnajua, daima nimemhurumia Yona, kwa sababu . . .

140 Watu wengi waonekana kama . . . Wao husema, "Mkono wangu umelemaa. Vema, niliombewa, hamna tofauti." "Tumbo langu linauma, hamna tofauti." Maadamu unaangalia hilo, hutakuwa tofauti hata kidogo, huna budi kuangalia yale aliyosema Mungu.

141 Hapa wakati fulani uliopita, nilienda kuomba, yapata miaka kumi na mitano iliyopita, kwa ajili ya kijana mwanamume, amelala, akifa kwa dondakoo nyeusi, mama na baba wakinililia nije. Vema, ni—nikaenda kule, naye huyo daktari alikuwa daktari Mkatoliki, wala asingeniruhusu niingie, kasema, "Je, wewe ni mwanamume aliyeoa?"

Nikasema, "Naam, bwana."

"Una watoto?"

Nikasema, "Naam, bwana."

Akasema, "Siwezi kukuruhusu uingie," kasema, "huo huambukiza."

Nikasema, "Bwana, mi—mimi ni mhudumu wa Injili, mimi . . . "

Akasema, "Sijali," akasema, "huo huambukiza, huna chanjo yake."

Nikasema, "Vema, hiyo inaweza kuwa ni kweli, pia, lakini Mungu atanishughulikia."

Akasema, "Sikiliza, bwana," akasema, "siwezi kukuruhusu uingie."

Nami nikasema, "Vema, huku huyo mama na baba wamesimama pale wakilia, kwamba . . . "

Akasema, "Huyo mvulana yuafa, amekuwa mahututi kwa saa ishirini na nne zilizopita."

142 Nikasema, "Nataka kukuuliza jambo fulani, Daktari. Sasa, tunatofautiana ka—katika theolojia," nikasema, "wewe ukiwa Mkatoliki, na mimi Mprotestanti, lakini," nikasema, "tunamwabudu Mungu yeye yule, unapitia tu barabara tofauti. Lakini ningetaka kukuuliza jambo fulani: Kama huyo alikuwa

ni mvulana Mkatoliki aliyelala mle ndani akifa, naye padre alikuwa amesimama hapa, naye mvulana huyo alikuwa akilia, akimtaka, nao baba na mama wakiomba huyo mvulana apokee taratibu za mwisho za kanisa, ungemruhusu aingie?"

Akasema, "Mbona, bila shaka!"

Nikasema, "Mimi ni muhimu sana kwao, kadiri padre angekuwa kwake, huyo mvulana Mkatoliki."

Naye akasema, "Lakini ngoja kidogo, padre hajaoa, wewe umeoa."

Ndipo nikasema, "Kama niko tayari kutia sahihi taarifa kwamba na—nawajibika . . . Wala huo hautanipata."

143 Hatimaye nikamshawishi, naye akanivalisha kama Ku Klux Klan, na—na, kote usoni mwangu, nami nikaingia mle ndani, basi kulikuwako na maskini nesi mle, naye huyo mvulana alikuwa amepoteza fahamu kwa siku mbili. Nami sielewi chochote kuhusu dawa, lakini, kwa vyovyote vile, walimfanyia uchunguzi wa moyo, na *kitu fulani* ambacho kilishuka mpaka mkononi, naye alikuwa anaishi kwa shida, nasahau ni mara ngapi moyo wake ulikuwa ukidunda kwa dakika moja.

144 Na kwa hiyo, maskini baba na mama wamesimama pale, kasema, "Loo," akasema, "Mama, angalia, Ndugu Branham yupo hapa, itakuwa . . . Bwana ataponya sasa." [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

145 Nikamwombea, nikasema, "Baba wa Mbinguni, ninakuja hapa sasa, kama mtumishi Wako, ninakuja kwa imani, mimi . . . Uliniruhusu niingie kwa njia fulani, kwa hiyo mbali na daktari huyo, alijibana kidogo akaniruhusu niingie. Na sasa, ninaweka mikono juu ya mvulana huyu wa thamani, anayekufa, nami naomba arudishiwe maisha yake, katika Jina la Yesu Kristo." Nikainuka.

Ndipo mama na baba wakaanza kukumbatiana, wakisema, "Si ni ajabu hii, Mama?"

Nami nikasema, "Mnaamini?"

"Loo," kasema, "bila shaka!"

146 Kwa hiyo nikaendelea, nikaanza kutoka, ndipo maskini nesi akaenda pale. Nao walikuwa tu wakipaza sauti, na kumsifu Mungu kwa ajili ya uponyaji wa huyo mvulana, kamwe yeye hakusogea, naye huyo mama, maskini mama na baba wakishangilia.

147 Kwa hiyo, nesi akaja hapo, akasema, "Bwana," akasema, "Ninaamini ka—katika imani, mimi mwenyewe," akasema, "lakini mnawezaje kusimama hapo na kupiga mayowe namna hiyo, huku mtoto wenu wa pekee amelala hapa, akifa?"

"Loo," huyo baba akasema, "hafi, yu hai, ataishi."

"Mbona," wakasema, "Unawazaje chochote namna hiyo?"

Kasema, “Mbona, yeye yu hai, hakika.”

148 Akasema, “Sikiliza, bwana,” kasema, “ni vema kuamini, nasi sote tunaamini imani katika Mungu.” Mnaona, hapo unairudia theolojia hiyo chotara tena. Mnaona? Kisha kasema, “Lakini,” kasema, “wakati mkono huo . . . ” Chochote kile, sasa, endapo kuna daktari hapa, sijui ilikuwa ni nini, lakini kwa namna fulani, kamwe, wakati ulipowahi kushuka chini hivyo, mapigo hayo ya moyo pamoja na ugonjwa huu, hayajawahi kujulikana katika historia kamwe kurudi tena.

149 Huyo mzee mtakatifu akaikumbatia shingo ya maskini huyo nesi, akasema, “Kipenzi,” kasema, “umefundishwa kuangalia mtambo huo, huo ndio unaojua habari zake.” Kasema, “Sikulaumu, huo umefanya mambo mengi mazuri.” Akasema, “Lakini, unaona, inategemea kile unachoangalia,” kasema, “unaangalia yale mtambo huo usemayo, mimi ninaangalia yale ahadi ya Mungu isemayo.” Basi mvulana huyo ni mmishenari huko Afrika usiku wa leo, baba wa watoto wawili, akiihubiri Injili.

150 Inategemea kile unachoangalia. Biblia, Mkristo, huangalia Yasiyoonekana, si yale unayoona hapa, bali Yale Mungu aliyosema, ni ahadi. Sijali sayansi inasema nini ama chochote kile, ni Kile Mungu alichosema.

151 Mnajua, watu huzungumza kuhusu dalili, nafikiri Yona alikuwa na kisa kibaya sana cha dalili nilichopata kujua. Kumbukeni, alikuwa katika tumbo la nyangumi, na sasa, alikuwa huko mbali baharini kwa safari ya siku kadhaa, labda ilikuwa na kina cha mikono arobaini pale, ndipo dhoruba ikatokea baharini, nayo mikono yake ilikuwa imefungiwa nyuma yake.

152 Nanyi mnajua alichokuwa akifanya? Samaki anapokula, akishiba, anashuka chini chini ya bahari kupumzika. Mlishe tu samaki wako wa dhahabu uone kitakachotukia, anashuka kwenda kupumzika. Kwa hiyo, alikuwa na nabii huyu tumboni mwake, ameshiba kabisa, kwa hiyo a—akashuka aende kupumzika.

153 Naye huyo hapo huku mikono yake imefungiwa nyuma yake, na kama aligeuka katika matapiko ya huyo nyangumi, alipoangalia *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, *huku*, lilikuwa ni tumbo la nyangumi, kila mahali alipoangalia palikuwa ni tumbo la nyangumi. Sasa, hakuna mtu hapa katika hali hiyo mbaya usiku wa leo, mnajua hilo.

154 Lakini mnajua yale aliyosema huyo nabii? Alikataa kuona tumbo la nyangumi, akasema, “Ni ubatili wa uongo, sitaliangalia.” Akasema, “Lakini mara nyingine tena nitalitazama hekalu Lako takatifu.” Kwa maana wakati Sulemani alipoliweka lile hekalu wakfu, aliomba, mwanadamu, mtu wa duniani ambaye baadaye alirudi nyuma, na wakati

alipoweka wakfu hekalu la Mungu, aliomba, akasema, “Bwana, kama watu Wako wakiwa katika shida mahali popote, na watazame mahali hapa patakatifu na kuomba, basi sikia kutoka Mbinguni.” Aliamini sana hayo maombi ya Sulemani, mtu mmoja kwa hekalu la duniani.

155 Naye Mungu, sijui alilofanya, hapana shaka aliweka tangi la oksijeni mle ndani ama chochote kile, bali alimdumisha hai siku tatu mchana na usiku, na kumpeleka huko Ninawi, ambako alipaswa kwenda.

156 Na kama Yona angeweza kuamini hivyo maombi ya mwanadamu, mtu wa duniani ambaye baadaye alirudi nyuma, kwenye maskani iliyo ya dunia iliyojengwa kwa mikono, ni zaidi sana vipi, chini, sisi, chini ya hali *hizi*, tunaweza kuwa na imani katika Damu ya Yesu Kristo, Yule aketiye, sio kwenye hekalu la duniani, bali kwenye mkono wa kuume wa Mungu Baba kwa mavazi Yake Mwenyewe yaliyojaa Damu, akituombea tunapokiri! Ni zaidi sana vipi tunavyoweza kukana dalili yoyote ambayo ni kinyume na imani ya Mungu inayotuongoza! Tunawezaje kufanya jambo kama hilo? Sasa, nataka kuwaambia, Yona kwa jumla hakuwa hivyo, bali yeye, pia, Yona alikuwa katika mapenzi ya Mungu.

157 Sasa, hao watu walikuwa wameanza kuabudu hayawani na wanyama, hivyo ndivyo makafiri wanavyofanya, kuabudu wanyama. Ninawaona watu hawa wote, maskini hawa mbwa huku, wakipanga uzazi, naamini karibu limerudi Marekani, tena.

158 Kwa hiyo basi tunarudi, nasi tunaona ya kwamba wanaabudu. . .mungu wa baharini alikuwa ni nyangumi. Kazi yao ilikuwa ni uvuvi, wanaume wote walikuwa huko nje wakivua samaki kwa nyavu zao. Basi siku moja yapata saa tano mchana, huyu hapa mungu wa baharini anaingia, yule nyangumi, akainuka kutoka baharini. Wanaume wote wakaogopa, maana yule mungu mkuu wa baharini alikuwa akiingia. Akaenda mbio mpaka ufukoni, akautoa ulimi wake kwenye ubao wa kuingilia kwenye meli, ndipo huyo nabii akatembea moja kwa moja akitoka, na kuanza kutabiri, “Tubuni, la sivyo mahali hapa pataangamia katika siku arobaini!” Moja kwa moja akashuka barabarani, huku kichwa chake chenye upara kiking’aa, “Tubuni, la sivyo mahali hapa pataangamia! Tubuni, la sivyo mahali hapa pataangamia!” Hakika, huyo mungu akamtapika nabii, hakika. Mungu anajua jinsi ya kufanya mambo, Yeye anajua tu jinsi ya kufanya kila kitu kitendeke sawasawa.

159 Yesu alirejea kwake hapa, “Kizazi kiovu na cha zinaa kinatafuta ishara,” Yeye akasema, kinatafuta ishara. Lakini Yeye alisema, “Watapokea ishara, kwa kuwa kama vile Yona alivyokuwa katika tumbo la nyangumi siku tatu mchana na usiku, vivyo hivyo Mwana wa Adamu. . . ”

160 Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani, upesi sasa, maana naona hatuna budi kuharakisha, nataka kuwaulizeni jambo fulani: Alikuwa akizungumzia kizazi gani? Ni wangapi wanajua Maandiko sikuzote yana jibu maradufu? Hakika, yanalo. "Kutoka Ninawi...Kutoka Misri nimemwita Mwanangu," Mathayo 3, fuatilia nyuma rejeo hilo, alimwita mwanawe Yakobo, pia Mwanawe Yesu. Mnaona?

161 Vema, sasa, kama alikuwa akizungumza juu ya kizazi kiovu na cha zinaa, kilikuwa ni kizazi hiki, kizazi kiovu, na kibaya, cha zinaa, Naye akasema wangepokea ishara. Sasa, vaeni kofia zenu, vaeni, ufungueni moyo wenu, mbali na hayo wekeni faneli ya kiroho kulishika, kumbukeni, Yeye alisema, "Kizazi hiki kiovu na cha zinaa kitapokea ishara." Ishara ya namna gani? "Ishara ya ufufuo." Mnalipata? Kristo yu hai, usiku wa leo, miongoni mwetu, akifanya mambo yale yale aliyofanya. "Kizazi kiovu na cha zinaa kitapokea ishara ya ufufuo." Hivyo ndivyo hasa, vile hasa Maandiko yalivyoahidi, "watapokea ishara ya ufufuo."

162 Sasa, upesi kwenye mawazo yangu ya kufunga, laiti tungalikuwa na wakati zaidi, ila hatuna. Ndipo akamjia Sulemani. Katika siku za Sulemani...Sasa, nisikilizeni kwa makini sana kwa yapata dakika kumi. Katika siku za Sulemani, ulikuwa ni wakati wa ufanisi sana, Mungu aliipa dunia karama, ilikuwa ni karama ya upambanuzi. Sulemani alikuwa na upambanuzi. Ni wangapi wanaojua hilo? Naye angeweza kupambanua, kwa sababu ulitoka kwa Mungu. Neno la Mungu lilikuwa pamoja na Sulemani, angeweza kutambua. Vema, watu wote waliikimbilia karama hiyo, loo, jamani. Na mhudumu yeyote anajua huo ulikuwa—huo ulikuwa ni wakati wa ufanisi wa Israeli, hakuna vita, nao wakalijenga lile hekalu, na kila kitu kilikuwa na amani, na kila kitu, ule ufani-...maana walipokea karama ambayo Mungu alituma.

163 Wala siku hizo hawakuwa na televisheni, Bwana ashukuriwe, lakini wao, nao...jinsi pekee walivyoweza ku—kueneza habari ilikuwa ni mdomo kwa sikio. Na kila msafara upitao wangesikia kuhusu karama hii kuu, wangehudhuria kanisa la Sulemani na kuiangalia, kisha warudi na kuisambazia nchi, mpaka sifa zake zikaenea kila mahali.

164 Huko chini kabisa katika Sheba, weka alama kwenye ramani yako ni umbali gani, moja kwa moja kupitia kwenye Jangwa la Sahara, watu wakipita, kule chini kulikuwako na maskini malkia mmoja kule chini, naye akasikia sifa hizo. Kila mpitaji, angepitia Misri akisema, "Loo," ama, kupitia Israeli, angesema, "laiti ungalipanda kwenda Israeli. Loo, Mungu wao ni Mungu aliye hai, Yeye anatembea miongoni mwao. Wanaye mtu huko juu, ametiwa mafuta na Roho Wake, naye anafanya mambo ambayo mwanadamu hawezi kufanya, ni ya kimbinguni." Ndipo maskini huyo malkia akaanza kusikia habari zake, kila mtu akinena habari zake.

165 Vipi kama tungeendelea tu kuzungumza juu ya Mungu wetu namna hiyo, jinsi anavyomtoa Roho Mtakatifu, na amani, na furaha, ufahamu? Loo, si ingekuwa ni ajabu sana? Sasa, "Imani chanzo chake ni [Kusanyiko linasema, "Kusikia."—Mh.] kusikia Neno la Mungu." Sasa, maskini moyo wake ukaanza kuona njaa. Unajua, huwezi kuzungumza juu ya Mungu pasipo kuufanya moyo wako uwe na njaa, kama kuna chochote ndani yako, kwa vyovyote vile. Kwa hiyo, maskini moyo wake ukaanza kuona njaa, "Loo, sijui kama hiyo ni kweli?"

Msafara uliofuata ukapitia, "Je, mmekuwa huko Israeli? Wananiambia wana uamsho unaoendelea kule juu."

"Naam. Naam, naam, naam."

"Uliuona?"

"Naam. Loo, nawaambia, sijawahi kuona kitu kama hicho! Mbona, hakuna mwanadamu duniani aliyewahi kujulikana! Hekima hiyo, upambanuzi huo ni mkamilifu."

"Uliuona?"

166 "Loo, ulitenda kazi juu yangu, najua ulikuwa mkamilifu. Mnaona? Hakika, ulikuwa ni ajabu. Loo, laiti ungaliuona. Loo, mtu huyo, yeye—yeye, mbona, isingeweza kuwa ni huyo mtu, ni—niliuhisi mkono wake, nilimpa mkono, anavaa nguo kama sisi, bali ametiwa mafuta na Roho wa Mungu, naye anampa Mungu sifa zote. Alisema Mungu alimpa karama ya kuwaongoza hao watu. Loo, jinsi kila kitu kilivyo na utukufu! Laiti ungaliiona."

167 Imani chanzo chake ni kusikia. Sasa, leo tungesema, "*Ah, hmm!* Sisi ni Wamethodisti. Sisi ni Wabaptisti. Hatuna uhusiano wowote na upuuzi kama huo, la." Hi—hiyo ndiyo sababu hatufiki popote. "Ati watakatifu wanaojifingirisha, kundi hilo la Wapentekoste? La! *Ah*, *phhh!* Hamna kitu kwa kundi hilo la watakatifu wanaojifingirisha." Mnaona, endelea mbele, jina letu liko kwenye bomu huko nje mahali fulani. Tu—tutalipata, tutapata thawabu, msijali, kwa hiyo basi, waliipata ile siku waliyomkataa Yesu, waliipata siku ile walipowakataa hao wengine, wakamkataa Nuhu, na kote kuendelea. Na Mungu hashindwi kamwe, Yeye ni yeye yule daima, kwa hiyo tutalipata.

168 Sasa, tunaona jambo la kwanza lililotukia. Sasa, hebu tuangalie tu kwa da—dakika chache zaidi. Sasa, maskini huyo malkia akaanza kuona kiu, akiona njaa na kiu. Yesu alisema nini? "Heri wenye njaa na kiu ya haki." Hata kama wanacho ama hawana, wanakionea kiu tu, umebarikiwa. Kwa hiyo, akasema, "Sina budi kwenda nione!"

169 Kwa hiyo sasa jambo la kwanza analofanya, hana budi kwenda kumwona m—mchungaji wake, askofu wake, mwajua, kabla hajaweza kuja, kwa hiyo, mwajua, yeye ni mtu mashuhuri, mwajua. Kwa hiyo, ninaweza kumwona akipanda juu, akisema, "Baba mtakatifu, wananiambia ya kwamba Waisraeli, huko juu,

wana uamsho unaoendelea, naye Mungu wao ameshuka, anaishi ndani ya mwanadamu, naye ana upambanuzi wenye nguvu, wala hakuna kitu kama huo."

170 "Binti yangu, *ahem, ahem,* mimi ni mchungaji baba kasisi, na kweli unafahamu ya kwamba kama kulikuwa na kitu chochote katika njia ya kimbinguni kikiendelea, kanisa letu lingekuwa nacho." Tungali tunao, mwajua. Kwa hiyo, "Usilipumbaze kundi hilo, hilo ni kundi lisilo na elimu kule juu. Ha—hakuna kitu kama hicho, hayo ni mazingaombwe tu, ni bure. Usipande kwenda huko."

171 "Vema," akasema, "Angalia, kama ilikuwa kanisani mwetu, basi kwa nini silioni kanisani mwetu?" Hilo ni swali zuri. "Mbona silioni? Sasa, nimekuwa hapa, naye nyanya yangu alikuwa mfuasi wa kanisa hili, nyanya na babu yangu walikuwa washiriki hapa, baba ya babu yangu na mama ya nyanya yangu walikuwa hapa, nasi hatujawahi kuona msogeo mmoja wa kitu chochote cha kimbinguni. Kwa hiyo sasa unaniambia haya yote, na sanamu hizi na kadhalika, nanyi mna vitabu vingi sana hapa, na theolojia chungu nzima, lakini siwaoni, bali wananiambia ya kwamba Kitu fulani ki hai huko juu," amina, napenda hilo, "Kitu ambacho ni halisi, Kitu kinachoweza kujizaa Chenyewe." Haleluya! Si chotara, bali kinaweza kutoa kitu sahihi.

172 Vema, akasema, "Sasa, binti yangu, sikiliza, unatambua ya kwamba una hadhi ya kijamii? Wewe ni wa kiwa-. . ., vilabu hivi vyote, na kadhalika, kama ukienda, unajua kitakachotukia?"

"Sijali kitakachotukia." Jamani, mwanamume au mwanamke anapoanza kumwonea Mungu njaa, hakuna kitu kitakachowazuia.

173 Anarudi chini, laiti tungeweza kukaa muda mrefu zaidi juu yake, lakini hatuna budi kuharakisha, kwa hiyo anarudi chini, naye akasema, "Unajua nini? Ninaenda kwa vyovyote vile, kwa hiyo sijali kama watanitenga, na kuondoa jina langu kwenye kitabu, ninaenda kwa vyovyote vile. Haileti tofauti yoyote, iwapo kanisa letu halishirikiani nao, hilo halimaanishi kitu, ninaenda kwa sababu Kitu fulani moyoni mwangu kinaniambia kuna Mungu aliye hai mahali fulani, nimeazimia kumwona." Amina.

174 Sasa, unapopata hilo, hakuna kitu kitakachokuzuia, hakuna baba watakatifu, wala maaskofu, wala chochote kile kitakachokuzuia, hakuna sherehe za kipagani, wala hakuna theolojia ya kujibunia, wala chochote kile, ikiwa Mungu anausukuma moyo mwako. Kama hausukumi, ole wako, Mungu na akurehemu.

175 Ndipo tunaona, akasema, "Vema, sasa, kama wakiondoa jina langu kwenye kitabu . . . "

Dada wote wakakusanyika, wakasema, "Wewe ni malkia."

176 Akasema, “Sijali mimi ni nani, sina budi kuitikia wito huu unaoita.” Kilindi kinapoita kilindi, hapana budi kuwe na kilindi cha kuitikia wito huo. Hiyo ni kweli. Kabla hakujawa na pezi mgongoni mwa samaki, ilibidi kuwe na maji, kwanza, apate kuogelea humo.

177 Kama mnaamini katika uponyaji wa Kiungu, je, mnaamini? Semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hiyo inaonyesha kuna uponyaji wa Kiungu mahali fulani, hiyo ni kweli, maana kamwe msingekuwa na shauku hiyo.

178 Nina mvulana mdogo, kutoka kwenye gazeti hivi majuzi, ambapo alikuwa akila vifutio kutoka kwenye penseli zake, naye mamaye akamkuta akila pedali kutoka kwa baiskeli. Wakampeleka kwenye maabara kuninii, ama, kliniki kumpima, wakaona kwamba maskini mwili wake ulihitaji salfa, aliipata katika mpira. Kwa nini? Hapo ndipo salfa ilipo, katika mpira. Mnaona, kabla hakujawa na shauku ya salfa, ilibidi kuwe na salfa kuitikia shauku hiyo. Kabla hakujakuwako na uumbaji, hapana budi kuwe na Muumba wa kuumba huo uumbaji. Haleluya!

179 Na endapo, usiku wa leo, tuko hapa tukiwa na njaa ya uponyaji wa Kiungu, kuna Chemchemi iliyofunguliwa mahali fulani. Ukiwa na njaa ya Mungu zaidi, kuna Mungu zaidi mahali fulani, la sivyo usingekuwa na hiyo njaa. Hiyo tu ndiyo sheria yake, ya Mungu, moja ya sheria Zake, kama vile kupanda na kuvuna, na kadhalika.

180 Angalieni sasa, akajiweka tayari, akasema, “Sasa, ngoja kidogo, huenda isiwe ni kweli, sijui, bali ninaamini ni kweli. Kwa hiyo, mwajua, kama ni kweli, nitachukua pesa nyingi sana, nitaliunga mkono, na iwapo si kweli, ninaweza kuzirudisha pesa zangu.”

181 Hilo, mwajua, lingewafaidi Wapentekoste kuchukua ushauri wake. Watu wengi sana wanaunga mkono mambo kwenye redio yanayowacheka, na kuwaita mtakatifu anayejifingirisha, inawadhihaki, na hata hivyo mnaunga mkono vipindi vya redio vyenye upuuzi kama huo, kwa pesa zenu nzuri, mlizopata kwa jasho. Ningeziweka mahali zinapofanya mema. Hiyo ni kweli. Wahudumu kamwe hawakuniambia niseme hivyo, sizungumzi na mtu yeyote wakati wa mikutano, niko peke yangu vyumbani. Lakini hiyo ni kweli, kama ni ya kweli, haistahili tu pesa zako, inastahili uhai wako, inastahili kila kitu. Kama si sahihi, achana nayo.

182 Kwa hiyo, ninawazia alinunua magombo yote, na kujaribu kusoma kile Yehova alichokuwa. Hiyo ni njia nzuri, tafuta kujua kile Yeye alicho, ndipo uone kama ni Yeye ama siye.

183 Hivyo ndivyo watu wanavyopaswa kufanya siku hizi, kusoma kile Yesu alichokuwa jana, kisha waone kama ni Yeye leo. Hiyo ni kweli. Waangalie kama Yeye hutenda vile vile leo

kama alivyotenda jana, waone kama ni Roho yeye yule, Mungu yeye yule kote katika Biblia, waone kama Ndiye, waone kama Yeye huonyesha mambo yale yale, ndipo iwapo theolojia yako ni kinyume na hiyo, ondoa theolojia yako na umchukue Mungu. Hiyo ni kweli.

184 Sasa, kumbukeni sasa, angalieni, alikuwa na hatari nyingi za kupitia, maskini malkia huyo alikabiliwa na mengi. Kumbukeni, yeye alifanya nini? Labda alijitafutia jeshi dogo, kundi la matowashi, na wanawali waende pamoja naye. Basi kumbukeni, alikuwa na safari ndefu ya kufanya. Isitoshe, watoto wa Ishmaeli walikuwa jangwani, nao walikuwa ni wanyang'anyi. Vema, hilo lingekuwa jambo rahisi jinsi gani kwa yote hayo. . . Alikuwa amechukua dhahabu nyingi, viungo ambavyo hawakujua chochote juu yake, walimwengu wengine, na uvumba, na hazina nyingi za thamani. Mbona, maskini. . . hao Waishmaeli, hao wapanda farasi waendao kasi wangeweza kuingia mle, na kuliua kundi hilo dogo, na kuchukua pesa hizo, kisha waondoke, katika dakika chache.

185 Lakini mwajua, wakati kitu fulani kinaposogea moyoni mwako kumtafuta Mungu, hujui hofu yoyote. Unasema, "Naweza kutembea, Ndugu Branham?" Ukiwa kweli una njaa ya kutembea, Mungu anaweka jambo hilo moyoni mwako. . . Unasema, "Huenda nikakosea." Ati nini? Ati kukosea? Mungu atakupitisha hayo, kamwe usiwe na wasiwasi juu ya hilo, iwapo Mungu anakwambia moyoni mwako.

186 Sema, "Ndugu Branham, ni—ningetaka kuwa. . . Ningependa kuhubiri Injili yote, lakini—lakini naogopa kuhubiri, wangenitenga, wangeninyang'anya makaratasi yangu." Watupie, uanze kutembea pamoja na Mungu.

187 Nesi mmoja aliniambia hivi majuzi, kasema, "Ninaamini uponyaji wa Kiungu," lakini kasema, "wataninyang'anya cheti changu, kama nikininii. . . mtu yeyote anayekiri uponyaji wa Kiungu," huko juu hospitalini ambako niliwaombea watu fulani, wakaponywa, kasema, "kama nikiukiri, wangeondoa haki zangu za wauguzi, waninyang'anye leseni yangu."

188 Nikasema, "Hiyo ni leseni bandia, itupilie mbali na uchukue leseni halisi," Nikasema, "naam, mahali ambapo Damu ya Yesu Kristo imeandikwa." Hiyo ni kweli. Chochote. . . Ninaamini katika dawa, ninaamini katika madaktari, ninaamini katika hospitali, lakini usiwe mlokole, usikiuke mpaka, kujua ya kwamba mambo hayo ndiyo mambo pekee, Mungu Ndiye aponyaye, hayo ni ya maumbile tu.

189 Ninaamini katika mitambo, ninaamini katika magari, na ninaamini katika sabuni ya kunawia mikono yetu, na nguo tunazovaa, na mitambo na kadhalika, ninaamini hiyo, bali hayatazuia imani yangu katika Mwenyezi Mungu kujua ya

kwamba Yeye ndiye huyatoa, na kuyatuma kwangu. Hiyo ni kweli kabisa, hakika.

190 Sasa, tunaona, alikuwa na mengi ya kumpinga. Lakini mnajua, wakati mtu yeyote kweli anamwonea Mungu kiu, hakuna chochote kitakachowazuia. Aliendelea mbele. Sasa, kumbukeni, yeye hakwenda tu kwa dakika kumi na tano. Ulipima huo umbali? Unajua inachukua muda gani, ingechukua muda gani kuendesha gari? Vema, jambo la kwanza, ilimbidi kupitia kwenye Jangwa la Sahara. Wala hakuingia kwenye Kadilaki iliyoyoyozwa, la, bali alienda juu ya mgongo wa ngamia, ilimchukua miezi mitatu kufika, miezi mitatu. Si ajabu Yesu alisema, "Yeye atasimama katika kizazi hiki, na kukihukumu."

191 Watu wanaishi ng'ambo ya barabara hawatakuja, wana magari, na usafiri, na kadhalika, na bado! Hiyo inaonyesha. Atasimama pamoja na Marekani hii, na kizazi hiki katika siku za kufufuka kwake, na kulihukumu taifa hili, Yesu alisema hivyo, hilo linalifanya sahihi.

192 Hakuja kwa gari lililoyoyozwa, wala Kadilaki. Labda ilimbidi kusafiri usiku, pa—pamoja na huo msafara mdogo na wale matowashi wachache, bali alikusudia kuona kama hilo lilikuwa ni la Mungu au la. Kote njiani, akisoma, na iliwabidi kusafiri usiku, mchana wakalala kwenye oasisi ndogo, mahali fulani chini, pepo zikivuma, na kusoma magombo, kile Mungu alichokuwa na kile Yeye angeninii . . . kile angaliweza kutarajia, kama ilikuwa ni Mungu.

193 Basi hatimaye alipofika kule . . . Sasa, hakuja kukaa kama watu fulani huko Bloomington, ama kadhalika, alikuja, wataingia, waketi chini kwa dakika moja, "Nitaenda, mtu fulani, mjakazi wangu, *nanii* wangu, waliniomba niende, kwa hiyo nadhani nitaenda, lakini kama akisema jambo moja kinyume na yale ninayoamini, nitaondoka moja kwa moja." Hiyo inaonyesha ujinga wako, hiyo inaonyesha ulilelewa katika nyumba ya namna gani. Nililelewa kwenye nyumba ya mlimani huko Kentucky, lakini mama yangu alinilea vizuri kuliko hivyo, kutoa heshima. Kama nikija, ningekaa kusikiliza, la sivyo nisingekuja kabisa. Lakini kupanda moja kwa moja, na, "Kitu cha kwanza atakachosema nisichokiamini, mimi huyo nitaondoka." Haya basi, endelea moja kwa moja.

194 Halafu, lakini yeye alikuja kukaa. Hatimaye alipofika langoni, alifanya nini? Aliwapakua ngamia, akapiga hema lake, na kujiandaa kukaa hata atakaporidhika, akiyachunguza Maandiko, mpaka alipoyachunguza aone kama yalikuwa ni ya kweli ama si kweli.

195 Sasa, hivyo ndivyo tunavyopaswa kufanya. Si ajabu atakihukumu kizazi hiki, hana budi kukihukumu. Yeye ni . . . atakihukumu. Alikaa, sio kusema, "Vema, kama wakihubiri

zaidi ya dakika ishirini, ndugu, nimeondoka." Vema. Lakini alikaa siku baada ya siku. Alikuja kwa sababu kulikuwa na kitu Fulani moyoni mwake kikimvutia.

196 Unasema, "Lakini, Ndugu Branham, huenda ikamaanisha nitapoteza saa mbili za usingizi." Ilimaanisha ufalme kwake, bali ilimaanisha Uzima kwake pia. Mnafikiri mimi ni mkali, lakini sivyo nilivyo. Mnaona? Ninawatakeni tu mjue kweli.

197 Kwa hiyo akakaa pale, akawapakua ngamia wake, kisha akaketi. Ninaweza kuwazia, kesho yake asubuhi, mchezo mdogo wa kuigiza sasa katika kufunga, anaenda kwenye, ama, akasema, "Nitaona sasa. Ninajua karibu tu kile Yehova alicho, kwa sababu nimewasoma manabii, nami ninajua itakavyokuwa."

198 Vema, kengele za kanisa zikalia, nao muziki ukapigwa, baada ya kitambo kidogo Mchungaji Sulemani akajitokeza, akaja jukwaani, wakamwona wa kwanza aliyekuwa na kadi ya maombi, ama chochote walichokuwa nacho, akija, ambaye, jinsi walivyokuwa wamechagua, akapanda juu. Akaona kwamba upambanuzi ulikuwa mkamilifu, ninawazia maskini moyo wake ukaanza kupiga. Wa pili akaja, kamilifu; mwingine akaja, kamilifu; anayefuata akaja, kamilifu. Loo, jamani!

199 Ninawazia alirudi hemani mwake, akawaita maskini wajakazi wake waingie, kasema, "Loo, ni kweli kabisa, kulingana kabisa na Neno hili, Maandiko haya hapa ninayosoma, ni kulingana na yale wengine wote wanayoniambia. Nitajitafutia kadi, kisha nipande kule juu, pia. Naam, bwana. Kwa hiyo, nitaenda."

200 Kwa hiyo akapata kihusishi chake, ndipo alipofika mahali ambapo angepandia, akajitayarisha, hasa, basi alipokuwa tayari, alipofika mbele ya Sulemani, Biblia ilisema ya kwamba hakukuwa na kitu kilichofichwa Sulemani mbele yake, alimwambia yaliyokuwa moyoni mwake.

201 Mnajua kile maskini mwanamke huyo kafiri alichofanya? Aligeuka, kwa sababu Sulemani alisema hilo, naye alijua lilitoka kwa Mungu, akasema, "Ahimidiwe Bwana Mungu." Angalieni hayo maneno, Elohimu, Yehova mkuu, "Ahimidiwe Bwana Mungu wenu awapaye mambo haya. Yote niliyosikia yalikuwa kweli, na zaidi ya niliyosikia," kwa sababu yalitendeka kwake, mnaona, "zaidi ya niliyosikia ni kweli." Naye akasema, "Hata heri watu hawa walio pamoja nawe, wanaosimama hapa kila siku, wakiangalia mbele zako, kazi hii ya karama. Heri walio pamoja nawe. Loo, hili ni tukufu," akasema.

202 Naye Yesu alisema atasimama katika Siku ya Hukumu, na kukihukumu kizazi hiki, kwa sababu hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani. Ee Mungu, uturehemu, ndilo ombi langu.

203 Ningependa kuendelea mbele kidogo. "Heri watu walio pamoja nawe, ambao daima wanaona hili likiendelea sikuzote.

Yote niliyosikia ni kweli, na zaidi, kuna zaidi ya nilivyowazia, ni ya kweli."

Na tuinamishe vichwa vyetu.

204 Bwana Yesu, Wewe ungali ni Mungu yeye yule, hakuna tofauti ndani Yako. Wewe ni Mungu juu ya paa la nyumba, Wewe ni Mungu mlimani, Wewe ni Mungu bondeni, Wewe ni Mungu wa bahari, Wewe ni Mungu wa mbinguni, Wewe ni Mungu wa Maumbile, Wewe ni Mungu wa maisha yetu, Wewe ni Mungu wa kila kitu kilichopo, Wewe ni Mungu. Ninakuomba Wewe, Bwana, ya kwamba kama kundi hili dogo la watu, watu mia mbili ama mia tatu tu wanaoketi hapa pamoja, usiku wa leo, hata hivyo Wewe ulikuja kote kutoka Mbinguni kusikia kilio cha ombaomba mmoja kipofu, ulikuja kote kutoka Mbinguni wakati mmoja kujibu, ama, kuvuka bahari kwa ajili ya mtu mmoja aliyekuwa mwendawazimu, yule mwendawazimu wa Gadara, ukamponya mtu huyo mmoja kisha ukarudi nyumbani Kwako, Wewe ungeru-. . . Ungetoka Utukufuni usiku wa leo, kulithibitisha Neno Lako, kwa sababu Biblia inasema Wewe huliangalia upate kulithibitisha.

205 Ee Mungu, na iwe kwamba hawatamwona maskini mtu huyu, asiye na elimu, bubu, anayesimama hapa akijaribu kunena Neno, lakini jalia Roho Mtakatifu mkuu aje na kunena. Wao ni kusanyiko zuri, Bwana, ninapenda kuzungumza nao, ninawaweka kwa muda mrefu sana kila usiku, lakini, Baba Mungu, Neno moja kutoka Kwako litamaanisha zaidi ya milioni moja, bilioni ambayo ningeweza kusema. Njoo, ukathibitishe ya kwamba yale niliyosema ni kweli, ya kwamba hapa yupo aliye mkuu kuliko Sulemani; njoo, ukawathibitishie, Bwana, ya kwamba Wewe ni Bwana Yesu aliyefufuka, ukilitimiza Neno Lako.

206 Ninajikabidhi mwenyewe, na kanisa hili, na watu hawa wagonjwa mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

207 Sasa, mtangojea dakika zingine kumi, ama kumi na tano? Si—sitakuwa na wakati. Basi yu wapi Billy Paul? Yeye. . . Alisambaza kadi gani Jumatatu, mnajua? Ama ile siku niliyotoa hiyo, Jumapili, ilikuwa hivyo, niliwaombea wagonjwa? Au zilikuwa. . .? Zilikuwa zipi? [Ndugu fulani anasema, "A, moja."—Mh.] A, A. Vema. Niliita kutoka ipi? Sehemu ya kwanza yao kuanzia moja? Hebu tuwaite kutoka sehemu yao ya mwisho.

208 Hebu tuone, hebu tuanzie, wapi? Hebu tuanzie kutoka sabini na tano. Hebu tuone kama tunayo. Ni A, moja. . . saba-. . . Je, A, sabini na tano iko hapa? Inua mkono wako. Mtu fulani angalia kadi yako. La? Vema, tutaanzia mahali pengine. Loo, sawa. Vema. A, sabini na tano, hiyo ni kweli? Njoo papa hapa, ewe kijana. A, sabini na sita, iko wapi? Vema, bwana. A, sabini na saba, inua mkono wako.

209 Tutawafikia wote, inatubidi tu kuwaita tuwezavyo. Sabini na saba, ilikuwa wapi? Sabini—sabini na saba, sabini na nane? Ni nani aliye na A, sabini na nane? Njoo hapa. Sabini na nane. Sasa, kuna kasoro mahali fulani. Sabini na tano, sabini na sita. Ni nani aliye na sabini na saba? Sabini na sita. Aisee, ni nani aliye na sabini na sita? Ni nani aliye na kadi ya maombi A, sabini na sita? Vema. Mtu fulani aliinua mkono wake kwa makosa. Usifanye hivyo, unatuchanganyisha. Vema, sabini na sita, sabini na saba, sabini na nane, sabini na tisa. Sabini na tisa, inua mkono wako, tafadhali. Vema, themanini.

210 Sasa, ikiwa huwezi kusimama. . .Ninyi watu mlio kwenye viti vya magurudumu, mna kadi za maombi? Vema, si lazima uwe na kadi za maombi upate kuponywa, hawa ni watu tu wanaokuja jukwaani.

211 Sasa, sabini na moja, ama, nilianzia wapi sasa? [Ndugu fulani anasema, "Sabini na tano."—Mh.] Sabini na tano. Sabini na tano, sabini na sita, sabini na saba, sabini na nane, sabini na tisa, themanini, themanini na moja. Themanini na moja, inua mkono wako. Themanini na mbili, inua mkono wako, ukiweza. Themanini na tatu, themanini na nne, themanini na nne? Vema. Themanini na tano, themanini na sita, themanini na saba, themanini na saba.

212 Mwangalie jirani yako, huenda ikawa ni kiziwi, wala hawezi kusikia, angalia kadi ya jirani yako. Angalia katika viti-. . . Wapi? Mmeipata? Vema. Themanini na saba, themanini na nane, themanini na tisa, tisini, tisini na moja, mbili, tatu, nne, tano. Moja, mbili, tatu, nne, tano. Tisini na sita, tisini na saba, tisini na nane. Tisini na nane, tisini na nane. Hivi mimi. . .? Niliikosa. Tisini na nane, inua mkono wako, tisini na nane. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

213 . . .kadi ya maombi. Nawe ni mgonjwa na unataka Mungu akuponye, inueni mikono yenu, inueni mikono yenu, popote. Kila mahali.

214 Sasa, tafadhalini, msiharakishe. Hebu, nyamazeni tu kwa dakika chache tu. Mtaninii—nyinyi. . .ita. . .Ni kitu gani kinachoweza kuwa muhimu zaidi? Kama ulimwengu ungesimama kimya, kama wangeunda bomu ambalo lingelipua ulimwengu wote, hilo—hilo lisingekuwa muhimu. Kama ulikuwa unaenda kupokea dola milioni mia moja, bado lisingekuwa muhimu. Mungu wetu yu hai? Je, imani yetu ni bure? Je, Yeye ni halisi, au Yeye si halisi?

215 Kama ningesema kuninii. . .? Kama—kama kila mmoja wa hao watu kwenye viti vya magurudumu walioketi hapo. . .Nafikiri sababu ya wa—wao kuingia, wameingia, watafanya maombi. Tunashuka kwenda kuombea viti vyote vya magurudumu kesho usiku, sivyo? Ama, ni lini, kesho usiku? [Ndugu fulani anasema, "Ijumaa usiku."—Mh.] Ijumaa usiku

wanautoa kwa ajili ya viti-. . .Hilo halininii. . .Haikubidi, unaweza kuponywa sasa hivi. Usingoje mpaka Ijumaa usiku, ninawapa changamoto kwenye hivyo viti vya magurudumu mwangalie huku, na kuamini ya kwamba mimi ni nabii wa Mungu, ama, samahani, mtumishi wa Mungu. Tafadhalini, mnaona, neno hilo huwatawanya, na kuwapiga watu, mimi si nabii, mimi ni mtumishi Wake tu. Amini hilo kwa moyo wako wote.

216 Siwezi kukuponya, la, bwana, wala hakuna mtu mwingine anayeweza kukuponya, imani yako mwenyewe ndiyo inayokuponya. Lakini kama utatambua ya kwamba ni Yesu yeye yule. Wakati alipokuwa hapa duniani, Yeye alisema, "Sifanyi neno mpaka Baba anionyeshe." Hiyo ni kweli, ninyi wahudumu? Yohana Mtakatifu 5:19. Yesu, vema wazieni, hakufanya mwujiza hata mmoja mpaka Mungu alipomwonyesha, si kumwambia, bali kumwonyesha kwa ono, la sivyo Biblia ilisema uongo, Yesu alisema uongo, kwa hiyo asingeweza kufanya hivyo, Yeye ni Mungu.

217 Yesu alisema katika Yohana Mtakatifu 5:19, "Amin, amin, nawaambia, Mwana hawezi kutenda neno Mwenyewe, bali lile amwonalo Baba analitenda, ndilo atendalo Mwana vile vile." Angalia kama hilo haliko katika Biblia yako, toleo la King James, ama Moffatt, ama tafsiri yoyote unayotaka kuchukua, tuone kama si jambo lile lile. Chukua Kamusi asili ya Kiyunani ukitaka, utapata jambo lile lile. "Sifanyi neno mpaka ninii. . . nitakapomwona Baba. . ." Kwa maneno mengine, Yeye aliigiza katika mchezo wa kuigiza.

218 Sasa, wakati tukiwaweka mstarini sasa, ninataka kuwaulizeni jambo moja. Angalieni, kulikuwa na mwanamke wakati mmoja katika Biblia ambaye hakuwa na kadi ya maombi, tutasema, lakini akasema, "Ninaamini ya kwamba Mtu huyo ni Mwana wa Mungu. Kwa hiyo kama ninaweza tu kugusa vazi Lake, nitakuwa mzima." Ni wangapi wanaojua hiyo ni kweli? Naye akagusa vazi Lake, hiyo ni kweli? Akarudi kwenye kusanyiko, labda aliketi chini, kama mlivyo ninyi, labda alisimama, sijui.

219 Lakini Yesu akasimama. Na kila mtu alikuwa akimkumbatia kwa mikono, mikono yao, na kusema, "Rabi, tuna furaha Wewe uko hapa." "Njoo, Rabi, tumesikia mambo mengi ambayo umefanya huko Galilaya, tungependa kukuona Wewe ukifanya jambo fulani huku." "U hali gani, Rabi? Njoo, nenda nyumbani pamoja nami kwa chakula cha kutwa."

220 Lakini maskini mwanamke huyo akapenya. Sasa, kimwili, Yeye asingeweza kuuhisi, kwa sababu vazi hilo linapwaya, tena lina vazi la ndani. Kwa hiyo, nisingeuhisi kama ungalikuwa nchani mwa koti langu hapa, kama tunavyoiita. Na vipi kuhusu

lile vazi kubwa, linalopwaya? Lakini Yeye aliuhisi kiroho, angalia yale aliyosema, Yeye alisema, "Ni nani aliyenigusa?"

221 Ndipo likamkasirisha Petro sana, akasema, akamkemea Yesu, Biblia ilisema ya kwamba Petro alimkemea Yesu, kasema, "Kwa nini useme jambo kama hilo? Vema, unasikika kana kwamba Wewe ni mwendawazimu. Mbona, kila mtu anakugusa, basi kwa nini useme jambo kama hilo?" akamkemea.

222 Akasema, "Naona kwamba nguvu zimenitoka." Hiyo ni kweli? Sasa, mnasoma katika toleo la King James, "Nguvu zilinitoka," ambazo ni uweza. "Naona kwamba nguvu zimenitoka."

223 Vema, kama ono moja, mtu mmoja alimfanya Mwana wa Mungu kutokwa na nguvu, ingenifanyia nini mimi, mwenye dhambi aliyeokolewa kwa neema Yake? Mnaona? Sasa, wakati Yeye. . .Huwezi kuchukua wengi kupita kiasi, unajua hilo, unaanguka moja kwa moja. Na wakati Yesu aliposema, "Mambo makuu kuliko haya myafanyayo," hebu chukua *Kamusi Mkazo ya Kiyunani* uone kama si kweli, "*Nyingi zaidi* ya hizi mtafanya," badala ya *kubwa zaidi*, "*zaidi*," usingeweza kufanya kubwa zaidi, bali ungeweza kufanya nyingi zaidi, maana kungekuwa na wengi zaidi, "mtazitafanya."

224 Sasa, ndipo akaangalia kote kwenye kusanyiko mpaka akamwona mwanamke huyo, Naye akasema, akamwambia ya kwamba alikuwa akitokwa na damu, na imani yake ilikuwa imemponya. Hiyo ni kweli? Sasa, ni wangapi wanaoamini ya kwamba Yeye angali ni Kristo yeye yule usiku wa leo? Ni wangapi wanaojua ya kwamba Agano Jipya, Ki—Kitabu cha Waebrania kilisema ya kwamba Yeye sasa hivi, dakika hii, ni Kuhani wetu Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu? Ni wangapi wanaojua hilo? Kama Yeye ni Kuhani Mkuu yeye yule, angetenda vivyo hivyo. Yeye ni Mzabibu, sisi ni matawi, Hawezi kufanya lolote, anatungojea tulifanye, alitufanya warithi pamoja, nasi ni watenda kazi pamoja Naye.

225 Sasa, wewe mguse kwa udhaifu wako, wewe usiye na kadi ya maombi, mguse Yeye, na kama nimewaambia yaliyo kweli, basi Yeye atajibu kupitia kwangu, na kukwambia jambo lile lile alilosema siku ile. Ni wangapi wangempenda, na kumwamini, na kumwabudu, na kumfia, kama angefanya hivyo, usiku wa leo, mbele zetu? Baada ya sisi . . . upambanuzi wa jambo hilo.

226 Baba wa Mbinguni, huo ndio umbali ambao mtu yeyote anaweza kwenda, linalofuata ni Lako, Baba, huna budi kunena Wewe, kwa kuwa siwezi kuongea zaidi. Sasa ni kwenye shindano la kuamua: Neno Lako ni kweli, ama si kweli? Na jalia watu hawa wote kwenye viti hivi vya magurudumu, watu hawa wote wenye ugonjwa wa moyo, watu hawa wote wenye TB, kansa, chochote kile, wajalie, Baba, waguse usiku wa leo. Jalia kila mtu

humu ndani aponywe. Ee Mungu wa Milele, ninamwombea kila mmoja wao.

227 Yasikie maombi yangu, Baba, ni—ninaninii tu, kwa moyo wangu wote, jinsi ningependa tu kukuona Wewe ukimponya kila mmoja, na, Baba, umemponya kila mmoja, ninaomba kwa ajili ya imani yao basi, ya kwamba haitashindwa katika saa hii, kwamba watajua ya kwamba hapajakuwapo na kitu kama hiki tangu siku za Kristo Mwenyewe, Nawe uliahidi itarudi katika siku hizi za mwisho, nayo hii hapa. Tujalie, Bwana. Ninakutegemea Wewe, nasema hilo kwa ujasiri, kwa sababu ninaamini ya kwamba Wewe utafanya, usiku wa leo, kama vile umefanya daima. Ninajikabidhi Kwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

228 Sasa, na ijulikane vizuri kwa kusanyiko hili, ya kwamba sidai kuwa Bwana wetu Yesu Kristo. Ni wangapi wanaelewa hilo? Yesu yuko Mbinguni. Atakapokuja, kila goti litapigwa, na kila ulimi utakiri. Lakini ninasema ya kwamba Roho Wake, Roho Mtakatifu yuko hapa, na kwa kipawa cha Kiungu cha huyo Roho Mtakatifu, nilipokuwa mvulana mdogo, mwenye umri wa miezi michache tu, niliona ono langu la kwanza, makumi ya maelfu ya hayo yametukia tangu wakati huo, wala hakuna hata moja la hayo lililopata kushindwa.

229 Ninazungumza na watu hapa ambao wamekuwa pamoja nami kote ulimwenguni. Basi inueni mikono yenu kama niliwahi kusema lolote katika Jina la Bwana, pasipo kutimia. Mtu yeyote hapa aliyewahi kunisikia nikitaja jambo fulani katika *BWANA ASEMA HIVI* ambalo kamwe halikuwa kweli, inueni mikono yenu kisha mje mniambie habari zake. Mnaona? Ni kweli. Basi ni Mungu, wanadamu hawawezi kufanya hivyo.

230 Basi kumbukeni sasa, ninyi watu mlio kwenye viti vya magurudumu, ninyi nyote, ama, ninyi msio na kadi za maombi, sio kama uko hapa au la, ambapo, mimi nikikugusa, haitakuwa na manufaa hata kidogo, wewe kunigusa mimi haitafaa kitu, bali kama utamgusa Yeye itatendeka, kwa sababu Yeye tayari ameununua uponyaji wako. Hebu tuwasikie mkisema hilo pamoja: "Tayariameniponya. Bwana, saidia kutokuamini kwangu nipate kuamini, na kumgusa Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wangu." Sasa, mmelipata, sasa kumbukeni.

231 Ninyi nyote katika mstari huo mnaojua ya kwamba sijui lolote kuwahusu, inueni mikono yenu, wote walio kwenye mstari huo wa maombi, kila mmoja. Wote walio katika kusanyiko wanaojua siwajui, wala chochote kuwahusu, inueni mikono yenu. Haya basi. Sasa, hii hapa Biblia inayosema jambo hilo, hii hapa Biblia ililiahidi, Roho Mtakatifu, na kama hili likitenda kazi, mnakumbuka, ambalo litatenda, kumbukeni, furaha hii

kuu mnayohisi, Kitu hiki kinachoitwa Roho Mtakatifu, hicho ni kweli.

232 Sasa, sikilizeni, kwenu ninyi Wapentekoste, hivi Paulo hakusema, "Kama mmoja wenu akinena kwa lugha wala hakuna mwenye kufasiri, mjinga atasema, 'Mbona, mna wazimu,' lakini akiwepo nabii miongoni mwenu, atakayetabiri na kuzifunua siri za moyo, ndipo wataanguka, na kusema, 'Hakika, Mungu wake yu pamoja nanyi'"? Hiyo ni kweli? Vema, kama unaamini katika kunena kwa lugha, unawezaje kukana jambo hili? Mnaona ninalomaanisha?

233 Sasa, wa kwanza ni nani? Ni nani . . . aliye mstarini? Huyu, ni wewe, ewe jamaa mdogo? Waweza kuja hapa? Mvulana mdogo, wazieni hilo. Sasa, sijawahi kumwona mvulana huyo maishani mwangu, nijuavyo mimi, hatufahamiani. Iwapo hiyo ni kweli, inua mkono wako, bwana, kwa Biblia hii. Sijawahi kumwona maishani mwangu, sijui lolote juu yake, lakini amesimama hapa kwa ajili ya jambo fulani. Labda yeye ni mgonjwa, sijui, sina habari. Kama yeye ni mgonjwa basi siwezi kumponya. Lakini nikiweka tu mikono yangu juu yake, niseme "Utaponywa, Mungu asifiwe, umeponywa, nenda ukaamini," vema, hilo ni sawa, kama angeamini, angeponywa, naamini, kama kweli aliamini, si imani ya kujifanya, bali kweli aliamini. Hivi huamini hilo? Mvulana huyo angeponywa.

234 Labda ni matatizo ya kifedha; labda yeye, ni matatizo ya kinyumbani, labda ameoa, naye na mke wake wana matatizo; labda yeye na mpenzi wake wa kike wana matatizo; labda hajaoa. Sijui yuko hapo kwa sababu gani, sina fununu, bali itahitaji Mungu wa Mbinguni kulifunua. Sasa, kama akifanya hivyo, kila mtu humu ndani atajua itabidi awe ni Roho fulani.

235 Huenda huyu mvulana ni mwanafunzi wa shule hii hapa, sijui, kama ndivyo, mimi . . . naye Roho Mtakatifu afanye jambo fulani kutoka kwake, ninatumaini ya kwamba angekuwa mwungwana vya kutosha kwenda awaambie. Mnaona? Hiyo ni kweli. Natumaini ndivyo ilivyo.

236 [Ndugu Branham anasumbuliwa na maikrofoni—Mh.] Samahani, loo, um, kitu hiki kwa namna fulani . . . Vema. Sasa, yeyote aliye kwenye maikrofoni, sijui. Wakati maono yanapogusa mnatambua ninaangalia mahali fulani, na kuona jambo lililotukia, na, huko nyuma kabisa mahali pengine, labda nirudi miaka kadhaa huko nyuma, na kadhalika.

237 Sasa, nitawaomba mwe na kicho kabisa. Roho Mtakatifu anapofanya jambo lolote, basi unataka kumsifu, hivyo ndivyo unavyopaswa kufanya, lakini wakati tukiketi, sasa hebu na tuingie kwenye Shekina kwa uchaji na kwa utulivu, Uweponi mwa Mungu, kwangu mimi na kijana mwanamume huyu hapa ambaye hatujawahi kukutana maishani mwetu, tukisimama hapa. Dunia . . . Watu hapa wanaoenda kwenye

Umilele kukutana na Mungu, na kujibu kwenye Siku hiyo ya Hukumu. Nasi tunaangalia kote katika Biblia Takatifu ya Mungu.

238 Wewe ni mtu ambaye, labda, baadhi yao walikupa kadi ya maombi, ndipo ikatokea tu kwamba usiku wa leo kwamba namba yako iliitwa, na hayo ndiyo yote unayojua kulihusu, tunasimama hapa. Na kama Mungu atanifunulia siri iliyo moyoni mwako na kukwambia, na kama Yeye ataniambia nikwambie kilichokuleta hapa, au shida yako, ama kitu fulani ambacho. . .ambacho unajua sijui chochote kukihusu, ungeamini kwa moyo wako wote, kijana mwanamume?

239 Je, kusanyiko lote lingeamini kwa moyo wao wote? Kwangu mimi na huyu kijana mwanamume, hawa hapa wanaume wawili wamesimama, watu wanaoelekea Umilele, juu ya Biblia ya Mungu iliyowekwa hapa. Mnaona?

240 Sasa, Bwana, ni juu Yako, ninaweza tu kunena Neno Lako. Nalo Neno Lako ni Kweli, nami ninalikaribia hili katika Damu ya Bwana Yesu Kristo, nikikiri hili nililohudumiwa na Malaika, ambalo haliwezi kushindwa, kwa sababu ni Mungu.

241 La, hutoki kwenye shule hii. Hata hutoki kwenye jimbo hili, umetoka nje ya jimbo, umetoka Missouri, ukaja hapa. Kweli. Wewe ni mhudumu, mhudumu kijana. Umechanganyikiwa kuhusu huduma yako, kile unachopaswa kufanya, hilo limekuwa moyoni mwako na niani mwako. Unajaribu kutafuta upate hata mahojiano ya faragha, pamoja nami, upate kujua la kufanya na huduma yako. Kaa mahali ulipo, Yeye anajiandaa kukusogeza. Unaniamini mimi?

242 Hili hapa jambo lingine, una mtu fulani moyoni mwako unayemwombea. Ni mwanamume, anakufa kwa kansa, nawe umesimama hapa kwa niaba yake. Mambo hayo ni kweli? Ni kweli. Unaamini sasa, unapata unachoombea? [Ndugu huyo anasema, "Naam."—Mh.] Basi nenda, amani ya Mungu iwe pamoja nawe.

243 Sasa hebu na tuinue tu mikono yetu. Enyi Wapentekoste, mnawezaje kutulia, wakati Mungu yeye yule mnayempenda ni mnyofu sana na ni wa kweli sana? Aminini tu. Hati zilizoapiwa! Roho Mtakatifu! Vema.

244 Sikujui, mama. Ninataka uniangalie kupitia hii Biblia. Sikujui, sivyo? Hatufahamiani, lakini kama Yesu Kristo atanifunulia, moyoni mwako, kama tu vile Yeye alivyozungumza na yule mwanamke kisimani, na angenifunulia jambo fulani unalojua. . .Kama ningalikuwa chochote, ni—nisingejua, kwa sababu unajua sikujui, wala hunijui. Mambo hayo ni kweli?

245 Unasema, "Unafanya nini, Ndugu Branham?" Ni Neno la Mungu *hapa* ndani ambalo ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mtambuzi wa mawazo ya moyo, Kristo, Neno lililo hai la Mungu, akijitambulisha Mwenyewe katika thibitisho lisiloweza

kukosea. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake, ama, mtumishi Wake?

246 Naam, wewe ni mgonjwa. Kama Mungu *atanielezea* mahali ugonjwa wako ulipo, utaamini? Uko kwenye mafigo yako, na katika kibofu chako. Hiyo ni kweli, inua mkono wako. Mmoja unasababisha huo mwingine, unatoka kwenye mafigo yako, mwasho kwenye kibofu. Ulipigana nao kwa muda mrefu, utakuacha sasa. Unaamini hilo? Hutoki mumu humu. Umetoka mji mwingine, lakini unatoka Illinois, Urbana. Hiyo ni kweli. U-. . .-b-a-n-a. Hiyo ni kweli, sivyo? Kama nikikwambia wewe ni nani, itakusaidia? Bibi Potts. Nenda ukaamini. Amini.

247 Unaamini kwa moyo wako wote? Hilo linapaswa kulitatua. Iweni tu na kicho, iweni na kicho kabisa. Tupe kama dakika tano tu zaidi. Mtu mwingine, tafadhali.

248 Njoo, angalia kote katika Biblia. Mungu wa Mbinguni anatujua sote wawili, Anajua ni kwa nini uko hapa, anajua ni kwa nini niko hapa, lakini kukujua wewe, sikujui. Sijui uko hapa kwa sababu gani. Lakini kama Mungu wa Mbinguni atanifunulia kilichokuleta hapa, utaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Basi, nisingeweza kukuponya, unajua hilo, bali itainua tu imani yako kwa uponyaji.

249 Ingewafanyia nini ninyi watu huko kwenye viti vya magurudumu? Angalieni tu, aminini tu sasa, saa yako imekaribia, iwapo tu utaamini sasa hivi.

250 Tafadhali msitembee huku na huku. Mnaona, kila mmoja wenu ni roho, nimewasiliana na kila mmoja wenu, kama pumzi, upako wa Roho Mtakatifu. Kila kitu ni chenye dhambi wakati hiyo inapokujia, kila kitu unachoangalia kina dhambi. Na kutokutii, hivyo ndivyo alivyoniambia, "Kama utawafanya watu wakuamini, na kisha uwe mwaminifu. . ." ninaposema, "Nyamazeni, msisogeesogee," wala hamfanyi hivyo, hiyo inaonyesha hamwamini. Mnaona? Na hiyo inaakisi tena kwangu, Roho Mtakatifu, anasema, "Waache, waache."

251 Lakini ninamlilia mchana na usiku, "Bwana, usifanye hivyo bado, jalia nijaribu tena," maana ninatambua Mbingu ni nini.

252 Je, uliwahi kusoma ule ushuhuda mdogo katika *Wafanyabiashara Wakristo*, kule kuhamishwa kudogo, ama, ono nililoona hivi majuzi usiku? Ninataka kila mtu humu ndani apate moja ya hayo. Kama huna pesa, lichukue haidhuru, nitalilipia. Mmelisoma? Hilo ni zuri? Ningewezaje kumwacha mtu akose Mahali hapo?

253 Una wasiwasi, matatizo, una shida nyingi, lakini kuna jambo moja muhimu ulilo nalo moyoni mwako, ni kwa ajili ya mtu mwingine, huyo ni mtu mwenye umri mdogo zaidi, ni mwanamke, ni binti yako. Ana wasiwasi sana, naye amefanyiwa upasuaji, huo ndio uliousababisha huo.

254 Wewe hutoki hapa, asili yake, umetoka Arkansas. Unaamini Mungu anaweza kuniambia wewe ni nani? Ingekusaidia? Bibi Martin, nenda nyumbani, Yesu Kristo anakuponya.

Amini, usiwe na shaka. Mwaminini Bwana.

Sasa, linanidhoofisha, Ndugu.

255 Tafadhalini, kila mtu, tafadhalini, nyamazeni, tulieni, tafadhalini, tafadhalini, tafadhalini. Naomba, tafadhalini, msisimame, tafadhali. Ninii tu, inaniacha, mnaona, ndipo basi sina budi kurudi tena. Mnaona? Tafadhalini, iweni tu na kicho. Vema.

256 Nadhani hatufahamiani, sivyo, bwana? [Ndugu huyo anasema, "Naam, hatufahamiani."—Mh.] Vema, bwana, hatufahamiani. Bwana Yesu anaweza kunifunulia shida yako ni nini, utaniamini? Ninachukia kuwaambia jambo hili. Unataka nikwambie haidhuru? ["Naam."] Umetiwa uvuli, kansa, umetiwa uvuli wa mauti. Ulikuwa na tabia fulani unazopaswa kuacha. Hiyo ni kweli. Utafanya hivyo? ["Naam, bwana."] Hebu nikuonyeshe jambo fulani. Nilihisi roho nyingine ikiingia, ibilisi. Unajaribu kujiweka sawa na Mungu. Kusema kweli, ndio kwanza ubatizwe, na kuwekwa sawa. Hiyo ni kweli.

257 Huyo mama aliyeketi hapo mwenye lukemia, unaamini Yesu Kristo anakuponya? Kama una imani, Yeye atafanya ninii... Unalikubali? Unaamini Yeye atakuponya na kukupa afya? Je, una kadi ya maombi? Huna? Unaona, ni kansa pia, Dada. Si lazima uwe na kadi ya maombi. Mwinulie Kristo mkono wako, useme...Huyo nama aliyeketi hapo na maskini koti jekundu miguuni mwake. Ambaye...

Je, ninyi nyote hamwoni hiyo Nuru ikining'inia juu ya huyu mwanamke?

258 Ninataka kukuuliza jambo fulani, kuwa mwaminifu kwangu. Nilipozungumza juu ya kansa na mauti, jambo la ajabu lilikupata. Hiyo ni kweli? Ulikuwa na kitu kama hisia ya kigeni, iliyokuja juu yako. Unaona? Je, hii ni kweli? Kama hiyo ni kweli, punga mkono wako kusudi watu hapo waone. Mnaona? Mnaona, ni mauti, pia, juu ya huyo mwanamke. Ni lukemia, ama hivyo ndivyo daktari alivyosema, naye amesema kweli.

259 Sasa, nyote wawili mko chini ya vivuli vya mauti, mchirizi huo mweusi unaotoka kwenye *huu*. Ni kitu gani? Ni yule ibilisi humu ndani anayeitwa *kansa*. *Kansa* ni neno la Kiyunani, ama, neno la matibabu, linamaanisha "kaa." Lakini ni ibilisi, ni mwuaji, mtesi, yuko juu ya mtu huyu, na katika mwanamke yule. Basi mnaona, alikuwa akiomba usaidizi kujaribu kumfanya mtu huyu kutokuamini, naye Roho Mtakatifu akamshinda kwa hilo, na kumtupia huyu mwanamke imani. Aligusa Kitu fulani. Mnaona, ibilisi huyo alidhani angeweza kupita nalo. Je, nyote wawili mtamwamini Yesu Kristo, na kumkubali kama Mponyaji wenu? Inueni mikono yenu. Basi katika Jina la Yesu Kristo,

ninamhukumu ibilisi huyo awaache nyote wawili, na kuondoka. Nendeni, mkapate afya. Nendeni, mwe wazima.

260 Kama kuna mtu yeyote hapa ambaye ana shaka, unapaswa kujionea aibu! Una hali mbaya zaidi kuliko walivyokuwa.

U hali gani?

261 Hivi hakuna bawabu hapo, kuchukua hizo kadi za maombi? Watu wanavuka wakiwa na, wakiwa na kadi zao za maombi mikononi mwao. Sasa, laiti mngalingojea tu kwa dakika moja ama mbili zaidi. Kusema kweli, tu—tuta—tu—tutaacha. Mimi...Mnaona, mnaposogea, mkisimama na kutembea-tembea, inatupilia mbali mawasiliano ya Roho.

262 Mnaona, Yuko kwenye kusanyiko. Mtu huyo aliyeketi hapo hapo mwenye yabisi kavu, unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Vema, bwana. Ulikuwa unaomba, sivyo, bwana? Angalieni jinsi alivyo mbali nami. Vema, amini kwa moyo wako wote, nayo yabisi kavu itakuacha.

263 Mwanamume aliyeketi papa hapa nyuma, wawili au watatu nyuma yake hapo, ana ugonjwa wa tezi kibofu. Bwana, ulikuwa ukiomba, ndipo Kitu fulani kilikuwa kimekugusa, nilipomwambia mtu yule yabisi kavu, Kitu fulani kilikugusa. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako, mtu kwa namna fulani mwenye upara, aliyevaa miwani. Hiyo ni kweli kabisa. Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Basi ninatangaza ya kwamba umeponywa, katika Jina la Yesu Kristo.

264 Mtu huyo papo hapo nyuma yake alikuwa na imani nyingi sana wakati huo. Hiyo ni kweli. Sikujui, bwana, lakini unaugua wasiwasi na magonjwa ya ziada. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Pokea uponyaji wako; Yesu Kristo anakuponya.

Kuwa na imani, usitie shaka.

265 Wasiwasi, anemia, shinikizo la damu. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli, mama? Inua mkono wako. Unakubali uponyaji wako? Vema, katika Jina la Yesu Kristo, wewe...

266 Kwa nini uliinua mkono wako huko nyuma, ewe mwanamke? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Unaamini Mungu anaweza kuniambia shida yako ni nini? Kwa moyo wako wote, utalikubali? Una ugonjwa wa kike wa akina mama, na ukurutu. Kama hiyo ni kweli, simama kwa miguu yako. Basi nenda nyumbani ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

267 Hivi hamwezi kuona ni Bwana Yesu? Ninampa changamoto yeyote wenu kuamini hilo. Hao watu huko nje, hawana kadi za maombi, wala chochote kile, wanaamini tu.

268 Unaniamini mimi kuwa ni nabii Wake? Ikiwa Mungu atanifunulia mambo yaliyo moyoni mwako...Mnaona, karibu yamenipata, kwa hiyo siwezi kukaa hapa muda mrefu zaidi.

269 Msininii, tafadhalini!

270 Niangalie, kama nilivyosema, kama vile Petro na Yohana walivyopitia kwenye lango liitwalo *Zuri*, kasema, "Tutazame sisi." Unaumwa na macho yako, unataka kuombewa. Bila shaka unasema, umevaa miwani, si hivyo tu, bali unaumwa na masikio yako, una tatizo kwenye pua yako ambalo huwezi kuona. Kama hiyo ni kweli, inua mikono yako. Hiyo ni kweli. Hawajui ni kitu gani, lakini kwa kweli ni kuvu, inaziba pua yako huko juu. Hiyo ni kweli. Na jambo lingine, una ugonjwa wa kifua. Hiyo ni kweli.

271 Wewe hutoki katika mji huu, hutoki katika nchi hii, umetoka Michigan. Hiyo ni kweli. Jina lako ni Bibi Swanson. Sasa, nenda nyumbani ukaponywe, katika Jina la Yesu Kristo.

272 Mnaamini, kila mmoja wenu? Basi wekeaneni mikono. (Kamwe siwezi kukaa jukwaani tena, inaniangusha . . .?. . .) Wekeaneni mikono, popote mlipo. (Tutasimama.) Wekeaneni mikono. Mbele za Roho Mtakatifu . . .

273 Kamwe siwezi kusimama muda mrefu zaidi, bila shaka ninyi nyote mmekuwa weupe huko nje, kama tu, ni Nuru tu juu ya kila mmoja wenu. Kama nimepata neema machoni penu, kama mnaniamini, ninyi mlio kwenye mstari wa maombi hapa, popote mlipo, kama unaamini kwa moyo wako wote, nami nimepata neema machoni pako . . . Roho Mtakatifu yuna kilindi sana humu ndani usiku wa leo, mpaka kuna Nuru kama kila mahali, siwezi kuwaona watu huko nje tena, inaonekana kumetiwa mafuta *sana*.

274 Kitu kimoja pekee kinachoweza kuwazuia msiponywe, hicho ni kutokuamini kwenu. Ninyi mlio kwenye viti vya magurudumu, popote mlipo, Roho Mtakatifu ameangaza mahali pote kwa nguvu Zake. Kwa nini msiukubali? Simameni!

275 Shetani, ninakukemea, ewe ibilisi, katika Jina la Yesu Kristo, Mwana wa Mungu. Ondoka kwenye kusanyiko hili, na uwaache!

61-0412 Aliye Mkuu Kuliko Sulemani Yupo Hapa
Illinois Wesleyan University
Bloomington, Illinois Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org